

Kitendawili

Phoenix, Arizona, USA
Januari 17, 1965

1 Mnaweza kuketi. Nimekuwa nikingojea muda mrefu kurudi hapa Phoenix. Hakika nina furaha alasiri ya leo kuwa hapa. Ninapokuwa Phoenix, kuna jambo fulani kuhusu hilo, daima hunifanya nijisikie kwamba nimeketi miongoni mwa watu ambao ni marafiki zangu, wanaonipenda. Na—na ni mashujaa wakuu wa maombi waliotoka hapa kuniombea, kwa miaka mingi. Daima ninakumbuka mkutano wa kwanza niliokuwa nao hapa na Ndugu Outlaw, Ndugu Garcia, na wahudumu hapa wa mjini. Jinsi ambavyo Bwana alibariki nilipokuwa tu katika ujana wa mikutano yangu! Tangu wakati huo, Phoenix imekuwa na ... Kitu fulani kiko moyoni mwangu, ambacho ni vigumu kueleza.

Kama mvulana mdogo, daima nilitaka kuja Phoenix. Daima nilisoma kuhusu jangwa. Nilikuwa na mashairi madogo niliyotunga juu yake, nilipokuwa mvulana mdogo tu, kuhusu Arizona.

Nina furaha sana kuwa mwe—mwenyeji sasa. Nadhani nina umri wa karibu mwaka mmoja, na labda zaidi kidogo. Bali hupati wengi sana walio na umri mkubwa kuliko huo. Kila mtu ninayekutana naye, ninasema, "Je! Wewe ni mwenyeji?"

"Vema, kadiri kulivyo nao. Nimekuwa hapa muda mrefu sana."

Na—na nafikiri ingewabidi kwenda kwenye hifadhi ya Apache, ama mahali fulani, kumpata mwenyeji halisi.

Na mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, unaonaje Arizona?"

Nikasema, "Vema, imekuwa moja ya matarajio yangu makuu ya maisha, ku—kuishi Arizona, na Mungu amenipa hilo."

2 Tuko hapa kabla tu ya mkutano wa Wafanyabiashara, ambao umekuwa ni kitu cha kila mwaka kwetu. Na alasiri ya leo, tunapokusanyika hapa kwa ajili ya mkutano wa kutangulia kabla ya mkutano huo ambao unaanza Alhamisi usiku, ninaamini. Imekuwa ni majaliwa yangu, kwa miaka michache iliyopita, kuja na kufanya mikutano hii midogo huku, kabla ya mkutano halisi kuanza kwenye...ama mkutano, hasa, unaanza.

Na Ndugu Williams ni rafiki mpendwa sana, yeye na Dada Williams. Hakika nina furaha sana moyoni mwangu kwa ajili ya watu hao. Wao daima wanalianika nirudi, na kwa hiyo tuna furaha kutimiza mwaliko huo alasiri ya leo.

Pia jukwaani, Ndugu Fuller, Ndugu Jewel Rose, na Ndugu Tony Stromei kutoka Tucson, na Ndugu Borders msimamizi wetu wa kampeni. Na n—ndugu mzuri wa thamani, Arganbright, tumekuwa pamoja katika vita vingi vikali. Kwenye ng'ambo ya pili ya mto; Ninatarajia kukaa pamoja naye ng'ambo ya pili ya mto huo mkubwa siku moja.

3 Siwezi kukumbuka jina la ndugu huyo, nimejaribu. Jina lako ni nani, ndugu? [Ndugu fulani anasema, "Al Booher." - Mh.] Booher, Ndugu Booher. Ni—ninajua uso wake. Na hivi wewe siye wakati mwingine anayewafasiria...["Kuwasiria viziwi."] kwa ajili ya viziwi. Hiyo ni ...

Nasi tuna furaha sana kuwa nanyi nyote hapa.

Nilikuwa tu nikiangalia hapa chini mbele yangu, nami ninawaona baadhi ya marafiki zangu kote kutoka Arkansas, hapa. Nilipokuwa hapa mara ya kwanza, niliwaambia ya kwamba kila mahali nilipoenda, nilimwona mtu fulani kutoka Arkansas. Nina hakika, kama nikipata kufika Mbinguni, nitawapata wengine kule kutoka Arkansas, maana hakika wamekuwa watu waaminifu, watiifu.

4 Na sasa, kwa kawaida mimi huzungumza kwa muda mrefu, bali nimejaribu niwezavyo kwa namna fulani kutengeneza Maandiko yangu na kuandika ili nisinene kwa muda mrefu sana. Nami nataka kuwaombea wagonjwa ninapokuwa Phoenix.

Sasa, Ujumbe ambao mimi ... Bwana amenipa, wakati mwingine, mwajua, mambo haya yanagusa sana. Na imekuwa hivyo katika kila wakati. Nami nimejaribu niwezavyo kudumu Nao. Ni kitu fulani. Na kama sikusema jambo lile ambalo Mungu aliniambia, na kama ilikuwa—isingekuwa ni la Mungu, basi Yeye... lisingekuwa kwenye Neno. Lakini kama liko kwenye Neno, na ahadi kwa ajili ya wakati huu, basi ninajisikia ya kwamba ninafanya yaliyo haki, kwa kuwa ninajaribu tu kudumisha kile alichohidi kwa ajili ya saa hii.

Na mara nyingi wakati usipokubaliana na mtu katika theolojia yao, mtakosana nao, upesi sana. Lakini hilo halipaswi kuwa. Ninajaribu kuninii ... Ninaona marafiki zangu ambao ni wa makanisa yote mbalimbali ya kimadhehebu, na kadhalika, kamwe sijagombana na hao ndugu. Jamani, ninaenda kwenye makanisa yao, kila mahali wanaponiruhusu kuja, na kuzungumza. Lakini hatupaswi kugombana, juu ya mawazo madogo.

5 Lakini, mnajua, kama nilisema kitu chochote tofauti na kile kilicho moyoni mwangu, ningekuwa mnafiki. Nami ni—ni ... Iwe mbali nami! Huenda ikanibidi kukutana Naye siku moja, kama mwenye dhambi,

bali hakika sitaki kukutana Naye kama mnaofiki. Lakini ninataka kuwa mkweli. Na kama nilisema tu, "Vema, nitaacha tu Hili kwa sababu hao wengine wanaamini *hili, lile,*" basi ni mtu wa namna gani? Msingeweza kuwa na imani kwangu, nami nisingekuwa na imani kwa Mungu wala kwa nafsi yangu, wakati nikipatana kwa urahisi jinsi hiyo.

Mtu yeyote hana budi kuwa na kitu fulani ambacho wana hakika nacho. Na hapo ndipo unapoweza kuweka msingi wa imani yako, ni wakati una hakika. Lakini mpaka uwe na hakika, kama kuna swali, liache mpaka uwe na hakika.

6 Sasa Billy labda ametoa kadi za maombi, ambazo nafikiri yeye ... Naam, nilimwambia afanye hivyo. Nami naamini aliniambia, muda mfupi uliopita, kwamba alikuwa ameniambia. Mahali fulani hapo, nitawaita wachache kwenye mstari wa maombi, baada ya kitambo kidogo, waombewe. Na kama kadi yako haiitwi ... Kama—kama ikiitwa, hasa, na huna hakika ya kwamba Mungu ndiye mponyaji na Yeye atakuponya, haitafaa kitu kuja hapa, kwa sababu hutaponywa. Wewe, kama kuna swali moja, unasema, "Vema, sasa, kama kuna jambo fulani maishani mwangu, kwa kweli ninapaswa kulinyoosha hili," nenda ukalifanye sawa, kwanza, kisha urudi kwenye mstari wa maombi, mnaona.

Kwa sababu, uponyaji ni mkate wa watoto. Tunatambua jambo hilo. Uko katika upatanisho, na upatanisho unatumika mioyoni mwetu kwanza. Na uponyaji daima umetangulia kila ujumbe, na pia umekuwa ni njia ya kuwakusanya watu pamoja. Na ni ninii ...

Watu wengi watadhamini mkutano wa uponyaji, wengi watakuja kwenye mkutano wa uponyaji, ama kwenye sikukuu ya nyimbo, lakini inapofikia maskini mtu aliyepotea kuokolewa, hakuna watu wengi wanaopendezwa na jambo hilo. Wao wananinii tu ... Lakini hilo ndilo jambo muhimu. Uponyaji wa Kiungu na sherehe za kuimba, na kadhalika, ni ninii tu ... Kama vile Ndugu Bosworth alivyokuwa akisema, "Ni chambo kwenye ndoana." Nawe unawaonyesha samaki chambo, si ndoana.

7 Na hilo ndilo jambo tu, kuwafanya watu wasikilize kwa muda kidogo, mpaka uweze kabisa kuwasilisha ujumbe wako. Mungu amefanya hivyo katika kila wakati, katika kila wakati, daima kumekuwa na kampeni ya uponyaji. Na kama ni kampeni halisi ya uponyaji, nyuma ya kampeni hiyo, daima, kuna ujumbe. Kamwe hakuna ishara iliyotolewa kwa ajili ya ishara tu; ni kutangulia ujumbe.

Nami naamini jambo lile lile ni, miaka kumi na saba iliyopita, ama miaka kumi na minane sasa, kwamba Bwana alinituma nianze kuwaombea wagonjwa. Ilifanya uamsho mkuu miongoni mwa watu. Watumishi wengi mashuhuri wa Mungu wamejitokeza na miamsho ya uponyaji, na, ila uamsho wa uponyaji, wenyewe, kama wewe ungali unakaa kwenye mwendeleo ule ule wa kale wa kile umekuwa sikuzote, kuna kasoro, uamsho huo wa uponyaji haukutumwa kutoka kwa Mungu. Hauna budi kuuvutia usikivu kwanza, mnaona, kuvutia usikivu, ndipo ujumbe unatolewa.

Yesu, wakati alipokuja, akiwaponya wagonjwa, na kadhalika, Yeye alikuwa ni Nabii mkuu kwa hao wote. Lakini wakati alipoanza kuwaambia Kweli, ya Injili, kwamba Yeye alikuwa nani na kile alichokuja nacho, basi Yeye—Yeye hakupendwa na watu baada ya hayo. Na hivyo ndivyo imekuwa daima katika kila wakati, na itaendelea hivyo.

8 Sasa tuko hapa alasiri ya leo, halafu kesho alasiri katika ukumbi huu huu. Yote ni kwenye saa moja. Hiyo ni kweli, ndugu? [Ndugu fulani anasema, "Saa moja na nusu." - Mh.] Saa moja na nusu, kesho alasiri, ama jioni, halafu Jumanne jioni. Nami nafikiri Jumatano jioni, pia. ["La, kwenye Hoteli ya Ramada, Jumatano."] Kwenye Hoteli ya Ramada, Jumatano. Na halafu Alhamisi, hiyo ni kweli, unanza ule—ule mkutano. Na kama Bwana akipenda, ninataka kuwa hapa katika hayo yote.

Niko hapa, ndugu yako, msaidizi katika Ufalme wa Mungu, kukusaidia kwa cho chote niwezacho. Kujibu swali lako, huenda nisingeweza kufanya hivyo. Lakini, kwa maombi, labda tungefahamu kama tungeomba juu yake na kumwendea Mungu juu ya jambo hilo, na tusitoe maoni yetu wenyewe.

9 Kama wewe ni mgonjwa, laiti ningaliweza kukuponya, bali hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo. Tayari limekwisha. Uponyaji umo ndani yako. Ni imani yako katika kazi zilizomalizika ambazo Mungu alifanya pale Kalvari, pamoja na Yesu Kristo. Na nje ya hayo, hakuna uponyaji; na nje ya hayo, hakuna wokovu; hakuna kanisa, hakuna dhehebu, hakuna ibada, hakuna kitu kinachobeba wokovu. Yesu Kristo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, makosa," samahani, "kwa kupigwa Kwake tulikuwa," wote katika wakati uliopita, "tuliponywa." Sasa, juu ya jambo hilo!

Sina ila dakika chache tu za kuzungumza, alasiri ya leo, kwenu, labda dakika ishirini, thelathini, halafu tutafanya mstari wa maombi. Kila siku, kama kawaida, watu wapya wanaingia, kwa hiyo kutakuwa na kadi mpya za maombi zitakazotolewa. Bali tutafanya yote yaliyo mikononi mwetu, yote ambayo Mungu ataturuhusu kufanya, kumwomba kila mgonjwa anayekuja, anayetaka kuombewa.

Kama kuna kitu kama mtu anayekuja kwa ndege, anayekufa, hali ya dharura ama kitu fulani, mbona, waweza kumwona Ndugu Williams, Billy Paul, ama baadhi yao kuwaingiza chumbani, kwamba hawataki

kuninii... Hawawezi kuketi, wanakufa, hawana budi kuhudumiwa sasa hivi, vema, waweke kwenye chumba fulani ili niweze kuwafikia mara moja.

10 Lakini ni bora zaidi, kama hauko kwenye hali hiyo ya dharura, kwamba wewe—kwamba wewe utachukua tu kanuni zako za imani na—na imani zako, na kuzisukumia kando tu dakika chache, muda mrefu kutosha tu kusikiliza yale Maandiko yasemayo, na halafu yale Mungu afanyayo kuhusu yale aliyoahidi. Na hiyo itajenga imani. Wala hata hutahitaji kuwa kwenye mstari wa maombi, ama mtu ye yote asikuombe. Tayari umeponywa, kama unaweza tu kuliadini. Mnaona? Na hilo ndilo kusudi lake, ni kukuacha wewe, ni kukufahamisha, wewe, yale ambayo Yesu amekufanyia.

Si lazima kuja hapa na kupiga magoti, na kuomba kwa bidii, mpaka u—mpaka umeokoka. Umeokoka tayari, bali huna budi kukubali jambo hilo. Kuomba kwako hakutoshi. Imani yako ndiyo inayokuokoa, si kwa maombi. Lakini, "Kwa imani unaokolewa." Jambo lile lile kwa uponyaji. Nina hakika sote tunafahamu jambo hilo.

11 Na iwapo kuna wageni malangoni petu, tunataka mjue ya kwamba, kwangu mimi, ama kundi hili nililo nalo hapa, Wafanya Biashara wa Full Gospel, hatuwakilishi dhehebu lolote. Tunawakilisha tu waamini Wakristo katika madhehebu yote. Kila mtu anakaribishwa. Tunafurahi kuwa pamoja nanyi. Unasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa fulani, je! Ningeweza kuombewa?" Hata haikubidi kuwa mfuasi wa kanisa, haikubidi kufanya lolote ila kuja hapa na kumwamini Mungu. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Mungu hufanya yaliyosalia.

12 Sasa, mimi—mimi...nimeichakaza Biblia moja, tangu nilipoanza katika miamsho ya uponyaji, ama kuwaombea wagonjwa, hasa. Huko Houston, Texas, nilipewa Biblia, miaka kadhaa iliyopita, miaka kumi na minane iliyopita, na Ndugu Kidson na kundi lake. Nami nilivaa Biblia hiyo, huku na huko, kote ulimwenguni, mpaka ikaisha kabisa, kurasa zikatoka kwake.

Nilikuwa tu nimepewa Biblia mpya. Na ajabu ni kwamba... Mimi si mshirikina; natumaini ninyi watu hamnidhanii kuwa mshirikina. Wakati nilipopewa Biblia hii, walikuwa na ninii ndogo ... alama mbili ndogo ndani yake, utepe mdogo. Ni Biblia kama niliyokuwa nayo.

13 Ndugu Kidson alinipa moja ilikuwa ni Biblia ya Scofield, sasa, si kwa sababu ninakubaliana na Bw. Scofield katika maandishi yake. Sasa, labda baadhi yenu mnakubaliana nayo, wengine wenu hamkubaliani, bali ninawataka mjue ya kwamba kamwe siichukui Biblia ya Scofield kwa kuwa ninaamini hayo. Kwa sababu, yeye ameigawa vizuri katika aya hata ninaninii... Hiyo ilikuwa moja ya Biblia zangu za kwanza, nami nilijifunza tu kusoma hivyo. Nami ninaIweka tu Biblia hiyo hiyo. Ambayo, kama ningalikuwa na ile ya Mfululizo ya Thompson, ingalikuwa ni nzuri zaidi. Ningaliweza kupata vifungu vyangu upesi zaidi kwenye ile ya Mfululizo wa Marejeo ya Thompson.

Lakini nilipoifungua Biblia, utepe mdogo wa kwanza katika Biblia ulikuwa ni kitu cha ajabu sana, mahali ulipokuwa. Ilikuwa ni wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu la Mungu, na Utukufu wa Mungu ulikuwa mkubwa sana, utukufu wa Shekina jengoni, hata makuhani hawakuweza hata kuhudumu.

Halafu uzi wa pili ulikuwa mahali ambapo Ezra alirudi na kuliweka hekalu wakfu.

Kisha kitia alama kidogo cha tatu, ambacho mke wangu alikuwa amenipa na kukiweka katika Biblia, bila kujua, kikiwa na jina langu, na kadhalika, kilikuwa kwenye Marko 11:22. Alikuwa tu kwenye Biblia, na hapo ndipo kilipokuwa, kwamba, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka.'" Nanyi nyote mnajua wakati Andiko hilo lilipokuwa mawazoni mwangu, ninyi watu wa kanda, hapo ndipo wale kindi wanapoingia moja kwa moja, katika ninii—ninii ... Hiyo ni kweli kabisa.

14 Halafu jambo la ajabu kwake lilikuwa, ndege ninayempenda sana, robini, picha yake ilikuwa kwenye alama, yule ndege mdogo mwenye kifua chekundu. Kama vile ile hekaya kuu isemavyo, kwamba wakati mmoja alikuwa ndege wa hudhurungi; bali kulikuwako na Mtu aliyekuwa akifa, siku moja, msalabani, naye akamhurumia Mtu huyo sana hata akaruka akaja kujaribu kuing'oa misumari hiyo yeye mwenyewe, naye akalowa damu kifua mwake mwote, na tangu wakati huo amekuwa na kifua chekundu. Hivyo ndivyo ni —ninavyotaka kumlaki Mwokozi wangu, pia, nikiwa na Damu Yake kwenye ninii yangu...ndani ya kifua changu, moyoni mwangu.

Halafu mkutano wangu wa kwanza, Ujumbe ninaopaswa kuhubiri hapa, uko huko Phoenix, Arizona. *Phoenix* ni kitu kinachoweza kuinuka kutoka kwa chochote. Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Yeye huchukua kitu kisichokuwa chochote, huinua kitu fulani kutoka kwake.

Na Ujumbe wangu alasiri ya leo, una jina, kwa dakika thelathini ama arobaini zijazo, "*kitendawili*." Nami ninataka kusoma kutoka kwenye Maandiko ambayo ...

15 Miaka michache iliyopita, ambapo, ningelitwaa Biblia, na niache unipe Biblia, wakati nilipoanza huduma yangu; na unachukua tu Biblia yako, na wengi wenu mmeniona nikifanya hivyo, ninaifungua tu namna *hiyo*, na kusema, "Bwana, U wapi Ujumbe wangu?" Ilifunguka kwenye Yoshua, mlango wa kwanza, Biblia

yoyote ungaliweza kunikabidhi.

Mpaka usiku mmoja ono likatokea, ambalo mnalifahamu, nami nikaiona Biblia hiyo ikishuka toka Mbinguni, na mkono wenye ukosi kwenye sijafu, namna *hii* ukashuka chini kwenye vifungu tisa vya kwanza vya Yoshua.

Hapo ndipo ninaposoma, alasiri ya leo, kwa ajili ya kusoma kwangu, ama kusoma Maandiko yangu. Somo langu linapatikana katika kifungu cha 10 na ninii—ninii ... Ninamaanisha sura ya 10 na aya ya 12.

Kabla hatujafungua Biblia, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Sasa huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, hebu na tufikirie jambo hili. Hebu na huu usiwe tu mkutano wa kawaida; tunayo hiyo kila wakati. Lakini hebu na tumwombe Mungu, kila mmoja wetu, ili jambo hili liwe la ajabu sana, hata kwamba Uwepo wa Mungu utakuwa pamoja nasi daima katika mkutano.

16 Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya majaliwa haya makuu na mazuri sana kuwa hapa Phoenix alasiri ya leo, tumekusanyika katika ukumbi huu mkubwa hapa, miongoni mwa watu hawa. Na sasa tuko karibu tu kulikaribia Neno. "Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Na jalia iwe tena, Bwana, ya kwamba Neno litakuwa mwili, litamiminika kupitia katika kanisa Lako na watu Wako, kutimiza ahadi za wakati huu.

Tunapotambua ya kwamba tuna—tunafunga wakati, wakati unakwisha. Inachanganyikana na Umilele. Nasi tuko kwenye Pwani ya Magharibi. Na kama vile ustaarabu umesafiri, Mashariki hata Magharibi, vivyo hivyo Injili imesafiri pamoja nao. Na sasa hakuna mahali pa kwenda ila kurudi Mashariki tena. Imekamilika.

Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hii itakuwa ni saa kuu kwa ajili yetu sisi sote, kwamba tuuhisi Uwepo wa Roho Mtakatifu, Mwandishi wa Neno hili, katika jengo la maskani ya mwili tena; akijidhihirisha Mwenyewe kwetu, katika kuzisamehe dhambi zetu, kusamehe uovu wetu, pamoja na hakikisho ya kwamba hatamhesabia mwaminio dhambi, pamoja na hakikisho la hiyo. Na pia kwamba atayaponya magonjwa yetu, na kuwaondoa wa—watu kutoka kwenye viti vya magurudumu na kutoka kwenye mikongojo; na kuwapa kuona, hao walio vipofu; na—na nyongeza ya siku, kwa hao wanaokufa kwa magonjwa mabaya sana kama kansa na kifua kikuu, mabaya, na magonjwa ambayo madaktari wetu hawawezi kuyazuia. Ni zaidi ya hayo, lakini, Mungu, Wewe huenda zaidi ya utafiti wote wa kisayansi. Unaenda zaidi ya hoja zote. Wajalie watumishi Wako, alasiri ya leo, kunena na kusikia Neno Lako, juu ya somo: *Kitendawili*. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

17 Sasa katika Biblia, Yoshua sura ya 1, na Yoshua sura ya 10. Sura ya 1 na kifungu cha kwanza.

Ikawa baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa Bwana, Bwana akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema,

Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli.

Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi, kama nilivyomwambia Musa.

Tangu jangwa hili na mlima huu, Lebanoni, mpaka mto ule mkubwa, mto wa Frati, nchi yote ya Wahiti, tena mpaka ... upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu.

Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha.

Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.

Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako.

Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.

Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.

[Ndugu Branham sasa anasoma Yoshua 10:12-Mh.]

Ndipo Yoshua akanena na Bwana katika siku hiyo ambayo Bwana aliwatoa Waamori mbele

ya wana wa Israeli; akasema mbele ya macho ya Israeli, Wewe Jua, simama kimya juu ya Gibeoni; Na wewe Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.

Ndipo jua likasimama kimya, na mwezi ukatulia, hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha jipatiliza juu ya adui zao. Hayo je! Hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka kuchwa kwa muda wa siku nzima.

Haikuwapo siku nyingine mfano wa siku hiyo katika siku zilizotangulia mbele yake wala katika hizo zilizoandama baada yake, hata ikawa yeye Bwana kuisikia sauti ya binadamu; kwa kuwa Bwana alipiga vita kwa ajili ya Israeli.

18 Bwana na aongeze baraka Zake katika kusomwa kwa Maneno Yake. Sasa somo alasiri ya leo: *Kitendawili.*

Sasa, neno *kitendawili*, kwa kuwa nimekuwa nikilitazama na kuwa na hakika ya kwamba—ya kwamba nilikuwa sahihi, neno *kitendawili* linamaanisha, kulingana na Webster, kwamba ni “kitu lisilosadikika, bali ni kweli.” Sasa, mwajua, tumesikia ule msemu wa kale, kwamba—kwamba, “Ukweli unaninii zaidi” (wanausemaje huo?) “ni wa kigeni zaidi kuliko hekaya,” ndivyo ukweli ulivyo. Kwa sababu, wakati mtu anaposema kweli, wakati mwingine ni wa kigeni sana.

19 Ninamjua rafiki yangu mmoja, ambaye, huko Kolorado. Walikuwa wanaendeleza hesabu, walitaka kuwahesabu kulungu. Basi kulikuwa na kulungu ishirini na mmoja kwenye kundi. Naye rafiki yangu, wakati, alikuwa amerudi huko kuwinda, wakati waangalizi walipokuja. Nao walikuwa wamelipa gharama kubwa, hifadhi ilikuwa imeilipia, kwa moja ya magari haya ya barafu, warudi wakawahesabu kulungu. Yeye alisema, “Hukupaswa kutumia pesa hizo zote. Ninaweza kuwaambia ni elki wangapi huko nyuma.” Nao wakamcheka tu. Kasema, “Wangapi?”

Akasema, “Kuna kumi na tisa.” Kasema, “Kulikuwa na ishirini na mmoja, nami niliwaua wawili wao.”

Na yule msimamizi akamcheka. Unaruhusiwa tu kumwua mmoja, mwajua. Naye akasema, akasema, “Naam, ninajua ulifanya hivyo.”

“Vema,” kasema, “hivyo ndivyo nilivyofanya. Kulikuwa na elk ishirini na moja, nami nikawaua wawili.”

Naye msimamizi akacheka tu na kurudi. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, elk kumi na tisa. Mnaona?

Yeye alinigeukia, akasema, “Unaona, mchungaji, sema tu ukweli, watu hawataamini.” Mnaona, sema tu ukweli, kwa hiyo ni jambo geni zaidi kuliko hadithi za uongo.

20 Yoshua hapa ni Kitabu, kwa kweli, ni Kitabu cha ukombozi, cha Agano la Kale. Yoshua, ingetupasa kukihesabu kuwa hivyo, Kitabu cha ukombozi. Kwa kuwa, ni, ukombozi una sehemu mbili. Ukombozi, mahali popote, una sehemu mbili. Hizo ni, “kutoka” na “kuingia.” Inahitaji sehemu mbili kufanya ukombozi, “kutoka,” “kuingia.”

Musa aliwakilisha torati iliyowatoa Misri, na, ambapo, Yoshua aliwakilisha neema iliyowapeleka katika nchi ya ahadi. Njia nyingine, ilikuwa, ile—torati na neema zilikuwa ni sehemu mbili mbalimbali za amri ya Mungu. Sasa, torati iliwatoa, Musa, na Yoshua akawaingiza.

Pia inawakilisha kitu fulani kwa siku yetu. Sasa inawakilisha, walivyokuwa safarini, wakitoka—wakitoka Misri kuingia kwenye nchi ya ahadi, vivyo hivyo nasi tumetoka ulimwengu wa Misri, machafuko, tukielekea kwenye Nchi ya ahadi. “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama isingalikuwa hivyo, ningewaambia,” Yohana 14. Kutoka “nje ya,” kuingia “ndani ya.”

21 Torati ndiyo inayotufanya tujue tumekosea, bali neema ndiyo inayotusamehe. Torati haina matumaini ya—ya ukombozi, kwa sababu...na kuikamilisha. Haina neema ndani yake, kwa sababu torati inaonyesha tu kwamba wewe ni mwenye dhambi, bali neema inakuambia jinsi ya kutoka humo. Sheria ni polisi aliyekuweka gerezani, bali ukombozi ndio uliokuja ukalipia faini yako; na “kutoka,” na “kuingia,” kuingia katika neema.

Waefeso. Sasa tunaona jambo lile lile, Agano la Kale, nafikiri Kitabu hiki cha Yoshua kinafaa. Neno linalofaa kwake, lingekuwa, Kitabu cha Efeso cha Agano la Kale. Kitabu cha Waefeso cha Agano la Kale, lingekuwa ni jambo zuri kukipa kitabu hiki Kitabu cha Yoshua, kwa sababu hakika kinafaa kwa hili.

22 Sasa tunaona Yoshua akiwakilisha neema, ama upatanisho, kwamba haingekuwepo kwenye wakati ule ule torati ilipokuwepo.

Wala ujumbe wowote, unaowapeleka watu mbele, kamwe haupatani na ujumbe uliopita. Hautapatana. Hautapatana. Hapo ndipo mlipo na shida leo hii. Yesu alisema, “Hivi mtu yeyote huchukua ki—kiraka kipya cha nguo na kukitia kwenye vazi kuukuu? Ama kuweka divai mpya kwenye viriba

vikuukuu? Huharibika. Huvipasua.” Haviwezi kuistahimili hilo.

Naye Yoshua hangeweza kamwe kuingia katika huduma yake mpaka baada ya Musa kuondoka. Kwa hiyo unaona aya ya kwanza kabisa hapa, “Musa mtumishi Wangu amekufa; sasa inuka na uwapeleke watu hawa kwenye nchi ya ahadi.” Musa, akiwakilisha torati, alikuwa ametumikia wakati wake. Ni, sheria ilikuwa imetumika wakati wake.

23 Walianza kutoka, kweli, kwa neema, kwanza. Kabla hawajapata sheria, walipata neema. Wakati wakiwa Misri, pasipo na torati; hakukuwako na mtu huko chini, ni makuhani tu, na kadhalika, bali hawakuwa na torati yoyote. Torati ilikuwa bado haijatolewa. Neema iliwapa nabii. Na, pia, neema ilitoa upatanisho, mwana-kondoo wa sadaka. Tutaingilia jambo hilo juma hili, juu ya sadaka, damu, kwa maana hapo ndipo penye uponyaji wenu. Kwa hiyo kwenye ... Upatanisho ulikuwa umetolewa kabla hapajakuwapo na torati yoyote. Neema ilikuwepo kabla ya torati, wakati wa torati, na baada ya torati.

Kwa hiyo huyo hapo Yoshua, akiwakilisha neema, alikuwepo moja kwa moja pamoja na torati, bali isingeweza kutumika mradi tu torati iko mahali pake hasa.

Na vivyo hivyo ulimwengu wa kanisa katika siku hii ya mwisho! Umekuja, umetumika mahali pake, bali wakati unakuja ambapo hauna budi kwisha. Haina budi kufanya hivyo. Hapana budi kuwepo na Waefeso, pia, ya safari hii, kama tu kulivyokuwa na ya safari zingine. Waefeso haina budi kuja, Waefeso, Waefeso ya safari hii. Angalia.

Ambapo sheria hiyo haingeweza kumwokoza mwenye dhambi, kama nilivyoeleza. Isingeweza. Kwa hiyo nchi ya ahadi iliwakilisha siku ya neema. Mnaona, asingeweza kuwaingiza, katika safari hiyo.

24 Na kama mliona, katika safari hiyo, walikuwa na hatua tatu za safari yao. Kwanza ilikuwa ni maandalizi kwa imani, huko Misri, chini ya mwana-kondoo wa sadaka. Ndipo wakavuka Bahari ya Shamu, wakaingia nyi—nyikani, utengano, ambao uliwakilisha hatua nyingine ya safari.

Maana, chini ya maandalizi, wakati wote walipokuwa tayari, basi walipofika kwenye—kwenye Bahari ya Shamu, palikuwapo na kushindwa tena. Watu hawakuamini, baada ya kuona mambo mengi ambayo Mungu alikuwa amefanya. Bado hawakuamini. Na Mungu akaifungua Bahari ya Shamu na kuwatoa, ambayo tunafundishwa ya kwamba watu wote walibatizwa kwa Musa, chini ya lile Wingu na bahari.

25 Sasa wao walibatizwa, wakatubu na kubatizwa, na wakaja kutembea katika maisha mapya, katika nchi mpya, katika safari mpya, miongoni mwa watu wapya, na mkono wa Mungu juu yao. Lakini hatimaye ilifikia mahali, katika mwendo huu waliokuwa nao, ambapo hawakuridhika na mwendo wao wa neema. Iliwabidi wafikie kitu fulani ambacho wangeweza kufanya wao wenyewe.

Sasa hapo ndipo watu wanapowazia, leo, juu ya uponyaji wa Kiungu, ama kazi nyingine yo yote ya neema, ya Mungu, ya kwamba kuna jambo fulani unalopaswa kufanya. Wewe, hakuna kitu unachopaswa kufanya ila kuamini, mwamini tu Mungu.

Na, wao, kama wangaliendelea! Ahadi hawakupewa chini ya torati. Ahadi ilitolewa kabla ya torati, pasipo na masharti yoyote kwake, “Nimewapa nchi hii, nendeni kule!” Lakini kabla hawajafikia ahadi hiyo, waliamua kulikuwa na jambo fulani walilopaswa kufanya wenyewe.

Na, kwamba, bado tunaona hilo miongoni mwa wanadamu. Tunapenda kuwa hivyo, “Kuna jambo ambalo hatuna budi kufanya.” Tunajisikia hivyo, kwamba tuna sehemu mle pia.

Kweli una sehemu mle, hiyo ni kuyasalimisha mapenzi yako, mawazo yako, kwa mapenzi na wazo la Mwenyezi Mungu, na imekwisha. Hakuna lingine. Chukua tu ahadi Yake, usifikirie kitu kingine. Tembea na Hilo, na Mungu hufanya hayo mengine.

26 Ndipo walitaka sheria. Na Mungu daima hukupa shauku ya moyo wako; Yeye aliahidi kufanya hivyo. Ila tunaona, walipopiga hatua moja kutoka kwenye upande wa yale Mungu aliyowaahidi awali, basi huo ulikuwa mwiba katika mwili mpaka torati ilipoondolewa, mpaka Yesu Kristo alipokuja na kusulibishwa kuiondoa torati. Ulikuwa ni mwiba mwilini.

Na chochote unachojaribu kufanya kwa nafsi yako, daima kitakuletea aibu. Kitakuletea matokeo mabaya. Mwamini tu Mungu tu, na hilo latosha. Kile Mungu alichoaahidi, “Mimi ni Bwana Mungu Wako Ambaye huonya magonjwa yako yote.” Mnaona? “Kama kuna ye yote miongoni mwenu, mgonjwa, na awaite wazee wa kanisa.” Yeye aliahidi, “Kazi alizofanya, zingefanywa katika kanisa Lake.”

27 Ni kwa nini inatubidi kuyakubali madhehebu, na kadhalika, ambayo yatafutulia hayo mbali kutoka kwenye Kitabu? Mnaona, ina—inakuwa mwiba katika mwili. Na hapa kwenye wakati wa mwisho, tunakabilia na jambo hilo tena, uso kwa uso, ni juu ya Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, na wowote wale, mnaona. Wewe, huwezi kuendelea; huna budi kurudi kwenye Injili yote kamili. Ilifanywa kwa ajili ya mtu mkamilifu, na Mungu mkamilifu aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Nasi tunajua ya kwamba mambo hayo ni kweli.

28 Sasa kama tukiangalia, basi, safari yao nyikani ndipo walipofanya kosa lao lililo kuu mno ambalo Israeli ilipata kufanya, mpaka Kalvari, lilikuwa wakati (katika Kutoka 19) waliikubali torati badala ya neema. Walikuwa na neema. Walikuwa na nabii. Walikuwa—walikuwa na mwana-kondoo wa sadaka. Walikuwa na ukombozi. Walikuwa wamepitishwa kwenye Bahari ya Shamu. Walikuwa wameponywa magonjwa yao. Walikuwa wamepata maji kutoka kwenye mwamba uliopigwa. Walikuwa na—walikuwa na mana kutoka mbinguni. Kila kitu walichohitaji walikuwa wamepewa, na bado walitaka kitu kingine.

Sasa huo ni mfano mkamilifu wa Waefeso wetu leo, hasa. Tulitoka chini ya Luther; tulipitia utakaso, chini ya Methodist; kisha akaingia kwenye kule kurudishwa, chini ya Pentekoste. Kama vile ilivyokuwa hasa, safari ya jangwani. Na wakati Mungu alipotutoa, tulifanya vizuri sana. Lakini tulifanya nini? Nilitaka kuwa kama hao wengine. Sasa tunaona ya kwamba neema ndicho kitu pekee kinachotufanikisha, kamwe si torati.

29 Yoshua hapa ni mfano wa huduma ya siku za mwisho. Mnaona? Sasa kumbukeni hizo hatua tatu za safari. Zote zilikoma, kwanza ilibidi torati na kila kitu kukoma, kusudi Yoshua... Nalo *Yoshua* ni neno lile lile kama Yesu, "Yehova-mwokozi," aliyewatoa kutoka nyikani mwao akawaingiza kwenye nchi ya ahadi. Sasa najua wengi hushikilia ...

Nami sitaki kupingana na wasomi, bali wengi wanashikilia ya kwamba nchi ya ahadi inawakilisha Mbinguni. Isingeweza kuwakilisha Mbingu. Isingeweza, kwa kuwa walikuwa na vita, na matatizo, na vurugu, na kila kitu, kwenye nchi ya ahadi. Haiwakilishi Nchi ya ahadi.

30 Lakini mnaona, kabla tu hawajaingia kwenye nchi ya ahadi, to—tofauti zote ambazo—ambazo zilikuwa zimeibuka miongoni mwao. Wao ... Moja ya mambo makuu ilikuwa ni Kora. Hakutaka uongozi huu wa mtu mmoja. Dathani, na jinsi walivyojitokeza mbele ya Musa na kujaribu kumwambia ya kwamba "ilibidi u—ujumbe umaanisha hili," na kuweka tafsiri tofauti kwake, mawazo yao wenyewe ya kile lilichokuwa. Nao kila mmoja wao aliangamia! Kila mmoja!

Yesu alisema, "Wote waliangamia."

Walisema, "Baba zetu walikula mana jangwani, kwa muda wa miaka arobaini," Yohana Mtakatifu 6.

Yesu alisema, "Na kila mmoja wao amekufa."

Mauti maana yake ni "Kutengwa Milele." Wote wamekufa, hata hivyo walifurahia kusikia ujumbe, hata hivyo walifurahia mana iliyoanguka. Si mana nyingine; ile mana halisi!

31 Lakini ilipofikia wakati ambapo Balaamu alitoka na mafundisho yake ya uongo, na kusema, "Sisi sote ni mmoja. Kwa nini tusiende pamoja na kuwaacha watoto wetu waoane wao kwa wao? Sisi ni taifa kuu. Tutawafanya wakuu pamoja nasi." Sasa mtu yeyote mwenye ufahamu wa kawaida wa kiroho anaweza kuona jambo lile lile hata leo, kuwaunganisha wote pamoja. Na ilikuwa ni dhambi isiyosameheka. Haikusamehewa Israeli kamwe.

Lakini basi Yoshua aliinuka kwa ajili ya kutoka.

32 Sasa tunafundishwa, katika Ufunuo sura ya 6, ninaamini, naam, sura ya 6, ya ile Mihuri Saba. Hilo linapaswa ... Kitabu hicho kufungwa kwa siri saba, ama Mihuri Saba, Ufunuo 6. Na katika siku ya mwisho, Ufunuo 10, katika Ufunuo 10, tunaona ya kwamba Laodikia, mjumbe wa mwisho wa wakati wa mwisho, na kwenye wakati wa unabii wake, ya kwamba Mihuri Saba ingefunguliwa, zile siri saba, siri zenye sehemu saba zilizokuwa zimeachwa.

Katika kila wakati kulikuwako na sehemu Yake iliyoachwa. Mtengenezaji hakuwa na wakati wa kuishughulikia. Katika siku za Luther, yeye alihubiri tu kuhesabiwa haki kwa imani. Alikuwa ameondoka, wakafanya kanisa. Baada ya hapo akaja Wesley, alihubiri utakaso. Huo hapo. Na halafu wakaja Wapentekoste.

33 Lakini tumeahidiwa, kulingana na Ufunuo 10, na kulingana na Malaki 4, na Luka Mtakatifu 22:17, na kadhalika, ya kwamba hatuna budi kuja Wa—Waefeso kwa jambo hili. Kuna jambo lililoahidiwa, enyi marafiki. Lazima Waefeso waje, kwamba hizi siri saba za Neno la Mungu hazina budi kufunuliwa. Na ni katika wakati wa Laodikia ambapo hili linatukia. Ninaamini ya kwamba tuko—tuko pale.

Ninaamini tuko moja kwa moja katika vivuli vya Kuja kwa Mwana wa Mungu. Na kama vile Yoshua, kabla tu ya Waefeso kuinuka, vivyo hivyo Yohana Mbatizaji alisimama kabla tu ya Waefeso wa pili. Nasi tumeahidiwa mwingine, Waefeso mwingine. Imebashiriwa hapa katika Maandiko, kwa hiyo nafikiri ya kwamba tunaishi katika Waefeso tena. Rudi tena kwenye ... Tumeahidiwa kwamba yale yaliyosalia katika zile nyakati saba.

34 Sasa huwezi kuongeza chochote kwenye Kitabu, wala kuondoa chochote kutoka Kwake. Ufunuo 22:18 yasema hivyo, "Atakayethubutu, atakayeongeza neno moja, au kuondoa Neno moja, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima." Sasa hatuwezi kuongeza wala kuondoa.

Kwa hiyo basi tunajua ya kwamba Luther asingeweza kulifikia; Wesley, na kadhalika, wale watengenezaji, Knox, Finney, Calvin, na kuendelea, na kadhalika, hawakulipata lote, bali waliyokuwa nayo ilikuwa ni Kweli ya Injili.

Lakini sasa katika siku za mwisho, tumefahamishwa, na Neno, ya kwamba tutalifahamu, kwa kuwa utakuja wakati wa Waefeso kwake. Nasi tuko hapa! Sasa, kitendawili! Nitaachilia hilo lining'inie, kwa kuwa nina yapata tu dakika kumi zaidi kisha tutafanya mstari wa maombi. Kitendawili! Kitendawili!

35 Kuna watu fulani, wa siku hizi, ambao hawaamini miujiza. Wanasema "hawawezi kuamini ya kwamba kuna kitu kama miujiza katika wakati huu wa kisasa." Vema, sikusudii kusema chochote kibaya kuhusu mtu huyo, bali hao wamekufa ganzi kiroho. Wao, wao, wao—wao ni vipofu kiroho. Hawana macho ya kiroho wala hisia za kiroho, hata kidogo. Maana, hakuna mtu anayeweza kuketi kwenye umati wa watu, ambamo Roho Mtakatifu anashuka, haidhuru mwanamume huyo ni mwenye dhambi kabisa, ama mwanamke huyo, pasipo kulazimika kuuhi Uwepo wa Mungu, mnapoliona Neno aliloahidi likitimizwa. Basi itabidi uwe umekufa ganzi; na unapoyaona kwa macho yako mwenyewe, yakitukia, basi itakubidi kuwa kipofu, kiroho, sineni kimwili. Lakini hakika unaweza ukawa kipofu kiroho, na kuwa na ishirini kwa ishirini, macho ya kimwili.

36 Mnamkumbuka Eliya kule chini Do—Dothani, wakati alipotoka na kulipofusha jeshi zima? Biblia ilisema alifanya hivyo. Ndipo akawaongoza moja kwa moja katika kuvizia, wakati hawakujua alikuwa ni nani. Na hata hivyo sura yake ilikuwa tu jinsi inavyopaswa kuwa, na kadhalika, naye akaenda moja kwa moja kwao. Lakini walikuwa vipofu.

Nawe unaweza kusimama katika Uwepo wa Mungu aliye hai, unaweza kusimama chini ya upako wa Roho na kuuona ukitenda kazi, na bado hautakugusa. Unaweza kuona yale Mungu aliyosema, yakihubiriwa kwako kikamilifu na kudhihirishwa, na hata hivyo hutaingia, "siliamini," basi, hapo, huwezi kufikika. Umekufa tayari, umekufa ganzi, umepofushwa, umekwisha. Walikuwa hivyo kabisa.

37 Ulimwengu. Nashangaa, kama mtu yuyo huyo asiyeamini katika mwujiza, sijui na kama yawezekana kwamba vitu pekee vinavyoweza, vilivyo halisi, ni vile vinavyoweza kuthibitishwa kisayansi? Sijui kama ungeweza kuwa na mwanasayansi yeyote, ama mtu yeyote asiyeamini katika mwujiza, kunielezea jinsi ulimwengu huu unavyosimama katika mzingo wake. Unadumishaje wakati wake mkamilifu, kuizunguka ikweta na vile unavyoenda, na ni mkamilifu kabisa? Hatuna mtambo, saa, au aina yoyote, inayoweza kudumisha wakati jinsi hiyo; itaachana kwa dakika chache kila mwezi. Lakini lile jua halichelewi kamwe. Lakini lile jua halichelewi kamwe. Maelfu ya miaka yanapita, halisogei; hakika, kikamilifu.

38 Jinsi ambavyo mwezi, mabilioni ya maili kutoka ardhini, ungali unaweza kudhibiti kupwa na kujaa kwa maji. Niambieni ambavyo katika kundi hili la nyota tunamoishi, mwezi ungewezaje kuathiri maji duniani? Kisayansi, niambie jinsi linavyofanywa. Isingewezekana, kwa maana hakuna njia yoyote ya kisayansi ya kulielezea. Bali Mungu aliuweka mwezi upate kuilinda bahari. Basi mwezi unapoanza kugeuka, dunia inapoondoka, hapa kwaja kupwa na kujaa. Lakini inapoamka, kesho yake asubuhi, ikiangalia *huku* nyuma, maji yanarudi mahali pake tena. Ni mlinzi.

"Loo," unasema, "hiyo ni kwenye ufuko tu wa bahari." La.

Hiyo ni papa hapa Arizona, moja kwa moja huko kwenye mkoa wa Kentucky, popote unapochimba shimo ardhini chini vya kutosha kupata maji ya chumvi. Utaona, maji yanapokupwa, hayo maji ya chumvi yanashuka kwenye bomba. Na wakati maji yanapoingia, pia yanaongezeka, mamia ya maili kutoka pwani ya bahari.

Tungeweza kuhubiri mahubiri juu ya jambo hilo. Jinsi ambavyo Mungu, haidhuru, Yeye yuko Utukufuni bali maagizo Yake kule yana matokeo yale yale ulimwenguni mwote na mtu yeyote anayeichukua ahadi hiyo. Agizo Lake linatolewa. Yeye ana kanuni za maumbile, na—nazo—nazo zitajiendeleza kikamilifu, kutoka kwenye Pentekoste ama wakati mwingine wowote. Wakati wo wote ambao Mungu alitoa ahadi, Yeye bado atadumu na ahadi hiyo bila kujali watu wako wapi, ni maelfu ya miaka mingapi. Sheria Zake daima zinabaki vile vile.

39 Jinsi mbegu inavyoanguka ardhini, nayo inaoza, na kuleta uhai tena. Inaonekana kama, endapo italetu uhai kamwe, ingekuwa ni wakati ikiwa katika umbo lake kamili. Kama uhai ulipata kuwa ndani yake, basi kwa nini usingekuwa tu? Liweke ardhini, uhai unachipuka. Ni kwa nini yote yanayouzunguka uhai huo, yote yaliyo karibu na chembe hai hiyo ambayo hamna mwanadamu anayeweza kuipata, ni kwa nini kila kitu kinachoshikika karibu na chembe hiyo hai hakina budi kufa? Ipate kuchipuka katika maisha mapya. Lakini kila kitu kinachoizunguka hakina budi kufa pia na kuoza, kabla haijachipusha uhai.

40 Ndivyo ilivyo kwa mtu binafsi. Mradi tu kuna nyongeza za mwanadamu, mawazo ya mwanadamu, basi chembe ya uhai wa Mungu, Roho Mtakatifu, haiwezi kutenda kazi. Huwezi kuponywa mradi kuna se—sehemu ndogo tu mahali fulani, ambayo bado haijaoza; ina elementi zote za binadamu, mawazo yote ya kisayansi, yote kuhusu "siku za miujiza zimepita," wanavyosema. Yote hayo hayana budi, yote, sio tu

kufa, bali kuoza, kisha kutoka hapo hiyo chembe ya Uzima inakua ikawa ni maisha mapya. Hivyo ndivyo tu inavyoweza kukua.

Hiyo ndiyo sababu hatupati tunachoomba. Tunajaribu kuchukua, pamoja nasi, mengi sana ya mawazo yetu wenyewe.

Hiyo ndiyo sababu kanisa la Kilutheri lisingeweza kusonga mbele zaidi kuliko lilivyofanya, Wapentekoste na hao wengine; maana wanaingiza, kwa kundi la wanatheolojia, "*Hili* halipaswi kuwa hivi. *Hii* ni kwa ajili ya siku nyingine. Na *Hili* lilikuwa kwa ajili ya hilo." Linabaki hapo. Haliwezi kukua kuifikia ile sura halisi ya Kristo mpaka kila Neno limepokewa ndani yenu, ndipo mnakuwa hilo Neno. Ni kama mbegu iliyoingia ardhini.

41 Ningetaka wao waeleze Waebrania 11:3. Mwanasayansi mkuu sana tuliyepata kuwa naye, nijuavyo mimi, alikuwa ni Einstein. Wakati nilipokuwa hapa si muda mrefu uliopita, huko New York, nilikuwa nikisikiliza yale aliyokuwa amesema. Naye alikuwa akizungumza juu ya kundi la nyota, na jinsi zilivyokuwa mbali, naye akathibitisha kwamba kulikuwako na Umilele. Jinsi ambavyo mtu, akienda maili milioni nyingi sana kwa saa, ingemchukua nyingi sana, ama maili milioni moja ya mbio za miaka ya nuru kwa saa, ingemchukua miaka mingi sana kufika kule, laki moja, laki tatu ama kitu kama hicho, na kisha laki tatu kurudi. Kisha akathibitisha kwa njia hiyo, kwa namna fulani, ya kwamba mtu huyo alikuwa tu ameondoka duniani kwa muda wa miaka hamsini! Umilele!

42 Na hilo ni kundi dogo tu la nyota, ambako Mungu alizipuliza kutoka mkononi Mwake! Biblia ilisema! Biblia ilisema! Naye Einstein hatimaye akamalizia na huu, "Kuna njia moja tu ambayo mtu yeyote anaweza kuelezea asili ya ulimwengu huu, hiyo inapatikana katika Waebrania 11:3. 'Tunafahamu ya kwamba ulimwengu uliumbwa pamoja kwa Neno la Mungu.'" Hiyo ni kweli kabisa. Sayansi hata haiwezi kuligusa. Na halafu unasema huamini muujiza? Ungewezaje kufanya jambo hilo?

Mwanasayansi yeyote angewezaje kuelezea mvua ya Nuhu, wakati hakukuwa na tone la mvua juu ya nchi mpaka siku hiyo? Lakini Nuhu alisema kungekuwa na mvua! Na wakati mvua ya Nuhu ilipokuja, kinyume na sayansi yote; hakukuwako na mawingu kule juu, hakujapata kuwa na mvua huko juu. Wangeweza kuthibitisha ya kwamba hakukuwa na mvua huko juu. Ndipo wakati Mungu alipozifungua mbingu na kuimwaga gha—gharika iliyoifagilia mbali dunia, hicho kilikuwa ni kitendawili; jinsi ambavyo hakika halieleweki, halielezeki. Lakini tunajua ya kwamba Mungu alifanya hivyo, kwa sababu Biblia ilisema hivyo. Nasi tuna ushuhuda duniani, leo, kwamba ilikuwa hivyo. Mungu alifanya hivyo. Hicho kilikuwa ni kitendawili.

43 Wakati Mungu alipomchukua mzee, jina lake Ibrahimu, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano; na mkewe, miaka sitini na mitano, miaka mingi imepita wakati wa maisha, kukoma hedhi. Na wakati alipomchukua mtu huyo na kumpa ahadi, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano; kwa mwanamke huyu ambaye alikuwa amemwoa, dada ya—yake. Naye alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa msichana; walifunga ndoa wakati labda alipokuwa msichana ti—tineja, na hapa alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Kisha akasema, "Utampata mtoto kwa mwanamke huyu."

Na vipi kama Ibrahimu angalisema, "Si—si—siamini katika vitendawili. Si—siwezi kukubali jambo hilo?" Isingalitukia kamwe.

Lakini, mnaona, unaposema unaamini jambo lo lote, basi huna budi kulitekeleza. Ndipo Ibrahimu aliamriwa kujitenga na kutokuamini kote, na kutembea na Mungu peke yake. Na badala ya kudhoofika, alipata nguvu zaidi. Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, na Sara alikuwa na tisini, mtoto huyo akaja.

44 Ibrahimu angewezaje kumchukua mwanawe, huko nyuma kabisa kwenye safari ya siku tatu, labda maili tisini kutoka kwenye ustaarabu wowote, kwenda juu ya mlima ambapo Bwana alikuwa amemwonyesha, aende akamtoe mwanawe mwenyewe, Isaka? Isaka akibeba kuni, kama tunavyojua, ambaye ni mfano wa Kristo. Na juu ya mlima huu alikuwa amtoe Isaka kama dhabihu, na hapo alipotimiza kila kitu ambacho Mungu alimwambia ila kuchoma kisu mwanawe hata kufa, kupitia kwenye koo lake, hapo alipokichomoa kisu kutoka kwenye ala yake na kuinua mkono wake apate kumtii Mungu, kwa neno! Kwa kuwa Biblia ilisema, ya kwamba, "Yeye alijua ya kwamba Mungu asingeweza kutoa ahadi isipokuwa Yeye aitimize. Naye alimpokea kama mtu aliyetoka katika wafu, kwamba aliweza kumfufua katika wafu na kumkabidhi huyo tena."

45 Ndipo alipokuwa tayari kumtii Mungu, kwa utimilifu wake, aliushika mkono wake na kusema, "Ondoa mkono wako, Ibrahimu." Naye huyu hapa kondoo dume aliyeshikwa nyikani, kwenye matawi, kwa pembe zake, juu ya mlima huo, ambako kuna simba, mbwa mwitu, fisi, mbweha, na wanyama wakali wakubwa mno wanaowala kondoo. Na halafu alikuwa huko juu juu ya mlima ambapo hakuna maji. Yule kondoo dume alifikaje kule? Ibrahimu alikuwa ameokota mawe kila mahali, kujenga ma—madhabahu. Lakini huyo hapo kondoo dume, hata hivyo. Ilikuwa ni kitendawili.

Na mtu ye yote anayemwamini Mungu na kumchukua katika Neno Lake, haidhuru hali ya mambo ilivyo, Mungu atafanya kitendawili kingine, kutimiza Neno Lake. Kwa kuwa, Ibrahimu aliita mahali pale *Yehova-Yire*, "Bwana amejipatia sadaka." Yeye angali anaweza kusababisha kitendawili kutukia. Anaweza kufanya hivyo alasiri ya leo, kama utamchukua tu kwa Neno Lake.

46 Danieli, kutoka kwenye pango—pango lililojaa simba wenye njaa, ingewezekanaje kwamba mtu huyo ... Ingewezekanaje kwamba mtu huyo, kwenye kundi la simba wenye njaa, alikaa pangoni pamoja nao, usiku kucha, bila madhara yoyote? Malaika wa Bwana, asiyeonekana kwa mtu mwingine yeyote, alikuwa amesimama pale. Ilikuwa ni kitendawili. Kitu fulani kilipaswa kumzuia huyo simba asimfikie.

Wakati wale wana wa kiebrania walipoingizwa kwenye tanuru lililowaka moto, hilo ni kinyume na ufahamu wote wa kisayansi, kwenye wakati huo mkuu. Ilikuwa ni jambo lisilo la kisayansi kwa mtu kutupwa katika tanuru, iliyokuwa, ambamo wale watu waliokuwa wakiwatupa humo waliangamia, nao wakaingia kwenye hiyo tanuru na kuishi kwenye tanuru hiyo kitambo kidogo, na jambo pekee ilichofanya lilikuwa ni kuwafungua minyororo yao. Hicho ni kitendawili. Lilikuwa halielezeki, halina sababu, bali hata hivyo ni kweli.

47 Huyu hapa Yoshua, ambaye tunanena habari zake. Jinsi ambavyo mtu huyo, mtu wa kawaida tu ambaye ndiyo kwanza apitie kwenye lu—lu—lundo la kanuni za imani ambazo watu hao walikuwa wametunga, na torati na sherehe, pasipo na kitu ndani yazo kinachosema kuhusu kumpa mtu nguvu kulisimamisha hilo jua. Lakini hapa, akiwa na agizo kutoka kwa Mungu, "Nitakupa kila kipande cha ardhi ambacho nyayo za miguu yako zitakanyaga. Nitakuwa huko." Naye adui akaangamizwa.

Jua lilikuwa linatua. Kama hao wafalme wangukuwa na wakati wa kujikusanya pamoja tena kesho yake, bila shaka angewapoteza watu. Lakini Yoshua alijua alihitaji nuru ya jua. Naye akaangalia juu kwenye jua, na kusema, "Simama kimya juu ya Gibeoni. Na, wewe mwezi, tulia hapo juu ya Aiyaloni." Na kwa muda wa siku nzima, huo ulikuwa usiku kucha, jua lilisimama kimya na mwezi ukasimama pale. Hicho ni kitendawili. Mtu anayetembea katika mapenzi ya Mungu angeweza kufanya jambo kama hilo, kwa maana alikuwa katika ninii ... alikuwa tena katika—Efeso, katika Wa—Efeso pamoja na—pamoja na Injili. Hakika, ilikuwa ni kitendawili.

Musa akiwa na fimbo mkononi mwake, kushuka kwenda kuwakomboa wana wa Israeli, ilikuwa ni kitendawili, huku Misri ikiwa na majeshi yote na watu wake waliofunzwa vizuri. Ilikuwa ni kitendawili.

48 Kuzaliwa na bikira kulikuwa kitendawili. Bikira angewezaje, kinyume na maarifa yote ya kisayansi, mwanamke asiyemjua mwanamume, angeweza kuzaa mtoto; wala si mtoto tu, bali Imanueli, ambaye alithibitisha kuwa kile hasa lilisema angekuwa. Hilo lingewezaje kutukia? Ilikuwa ni kitendawili. Kwa sababu, Mungu alinena na nabii Wake, mamia ya miaka hapo kabla, naye nabii alitii Neno la Mungu, nalo Neno likanena. "Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Nasi tunaamini jambo hilo. Hakika, ilikuwa ni kitendawili.

Jinsi ambavyo angeweza kutembea juu ya maji, hicho kilikuwa ni kitendawili. Mwanadamu, kulingana na ukubwa wa miguu yako, usingeweza kufanya hivyo. Lakini Yeye alifanya hivyo. Ilikuwa ni kitu gani? Haielezeki, bali ilikuwa bado ni kitendawili. Mungu alifanya hivyo. Tunaamini jambo hilo.

Kulisha watu elfu tano, na samaki wawili na biskuti tano? Lakini Yeye alifanya hivyo. Alizidisha si samaki tu, bali samaki waliopikwa; si mkate tu, bali mkate uliopikwa. Angewezaje kuyageza maji kuwa divai? Yote ni kitendawili!

49 Yeye aliwaponya wagonjwa, ambao, wenye ukoma. Ambao, hawana chochote, hata wa leo, sayansi haina, cha kuuponya ukoma, lakini Yesu aliuponya kwa Neno Lake. Ilikuwa ni kitendawili.

Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Neno Lake lingali linawaponya wagonjwa. Ni kitendawili, hakika.

Aliwafufua wafu, baada ya uhai wa kibinadamu kuwatoka; Lazaro, yule mwana wa yule mwanamke wa Naini, na binti ya Yairo. Yeye aliwafufua wafu, kwa Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Neno.

Na halafu jambo lingine kuu, katika kufunga, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Masihi. Kuthibitisha kile alichokuwa, ilimbidi kuja katika utaratibu, na kujibu, kwa Neno. Nalo Neno lilisema, wakati aliponena na nabii. "Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama mimi."

50 Kulikuwako na watu wengi walioinuka. Na kulikuwa na, kwa mamia na mamia ya miaka, hawakuwa na nabii. Loo, walikuwa na makuhani na watu mashuhuri, na tunaposoma historia kati ya wakati wa Malaki na Mathayo, miaka mia nne, kulikuwa na watu mashuhuri. Lakini hakukuwa na nabii.

Na ndipo i Yeye alipojitokezajukwaani, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Waefeso iliyodhihirishwa, Yohana alilitangaza hilo. Lakini Yesu alikuwa Ndiye, Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa, Mwenyewe.

Wakati Petro alipomjia siku moja, pamoja na Andrea, jina lake lilikuwa Simoni. Na wakati Yesu alipokuwa amesimama pale, kamwe hakumwona mtu huyo maishani Mwake, (sikilizeni kwa makini) wakati aliposimama pale na kumwangukia mtu huyo, na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hicho ni kitendawili. Hakika alikuwa. Hakika ilikuwa ni kitendawili.

51 Na wakati Filipo, akisimama pale, aliposikia hili na kujua kwa utambulisho wote kwamba huyu alikuwa Ndiye Masihi, hakika alikuwa. Yeye aliamini jambo hilo. Hakuwa amekufa ganzi, wala hakuwa kipofu. Akakimbia kote ufukoni, kwa maili chache, akampata rafiki yake, aliyetitwa Nathanaeli. Na wakati alipokuja akitembea ... Imani ya mtu huyo, ambayo ingeweza kumleta mwingine kwenye mkutano, kuona!

Wakati alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, "Tazama, yuko Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake."

Ilimshangaza mtu huyo. Yeye alisema, "Ulipata kunijua lini?" Sasa angalia, hili si la busara. Hali—halielezeki. Yeye alisema, "Ulipataje kunijua mimi?"

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Kitendawili!

52 Alikuwa na haja, kupitia Samaria. Na wakati alipopitia Samaria, mji wa Sikari, Yeye alikuwa ameketi pale akiwangojea wanafunzi Wake waingie kununua chakula. Na, angalia, mwanamke alikuja kisimani, mwenye sifa mbaya. Naye akamwambia, "Mwanamke, nenda ukaninyweshe maji, ama unilettee maji ninywe."

Naye akasema, "Si desturi Kwako kuomba hayo. Sisi ni, mimi ni Myahudi ... ama Msamaria, nawe ni Myahudi. Hatuna—hatuna uhusiano na Wewe."

Yeye alisema, "Lakini kama ulijua ni Nani unayezungumza naye!" Angalia kitendawili hiki kikielekea kutukia. Msikikose. Kasema, "Unawezaje—unawezaje kusema jambo hili? Mimi, mimi ni mwanamke wa Samaria, na Wewe ni Myahudi. Hatuna uhusiano."

Yeye alisema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayezungumza naye, ama ni Nani aliyekuwa akisema nawe, u—ungeniomba maji." Naye akaendelea mpaka akapata mahali ambapo shida yake ilikuwa. Naye akasema, "Nenda kamlete mumeo uje naye hapa."

Naye akasema, "Sina mume yeyote."

Yeye alisema, "Hiyo ni kweli. Huna mume, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako. Kwa hiyo, umesema kweli."

Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe u nabii." Hawakuwa wamemwona mmoja kwa mamia ya miaka. Kasema, "Tunajua Ma—Masihi yuaja, na, Yeye ajapo, Yeye atatuambia mambo haya."

Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

53 [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Ilikuwa ni kitendawili kilichothibitishwa, na imeonekana kuwa ni Kweli ya Injili; Injili iliyokuwa imeahidi jambo hili, na hili hapa likatukia na kuthibitisha ilikuwa ni nini.

Sasa hebu niwape kitendawili kikuu kizuri hapa, kwa dakika moja. Katika Yohana 14:12, Yesu alisema, aliahidi ya kwamba, "Mwamini aliyemwamini, atafanya kazi zile zile." Hiyo ni kweli? Mungu, ambaye hufanya torati ama ahadi, hana budi kutimiza ahadi hiyo, apate kuwa Mungu. Yeye huitimiza. Kufikiri, Mungu ... Mbona, Chenyewe, ni kitendawili; kwa Mungu, ambaye hutoa ahadi wala hawezi kuivunja ahadi hiyo, kutoa ahadi hiyo ya mambo aliyofanya, kwa watu Wake, kuyafuata kote katika nyakati mpaka atakaporudi tena. "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe; kila kiumbe, ulimwengu wote. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka, naye asiyeamini atahukumiwa; na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hana budi kulitimiza Neno hilo. Na kwa sababu Yeye alisema jambo hilo, lilitoka kinywani Mwake, halina budi kutimizwa.

Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Kwa hiyo ni kitendawili, peke yake, kumsikia Yesu, Mwana wa Mungu, akitoa tamshi kama hilo, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Sasa Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hicho ni kitendawili, maana hakina budi kufanywa. "Mbingu na nchi zitapita, bali hakuna Neno hata moja ambalo nimesema kamwe litashindwa," Yeye alisema. Halina budi kutukia.

54 Sasa, marafiki, ninaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini anaweza tu alasiri ya leo kusababisha, katika jengo hili, kitendawili, kwa sababu Yeye aliahidi lingetukia.

Basi ni mengine mengi zaidi jinsi gani Yeye ameahidi, ni zaidi kiasi gani yanayoelekeza katika Biblia, kwenye wakati huu tunaishi, Waefeso tena, ya nyakati za kanisa. Tuna nyakati saba za kanisa, na tumeahidiwa ya kwamba katika Wakati wa Kanisa la Laodikia kungekuwako na Waefeso nyingine. Hiyo ni kweli. Nasi tuko hapa. Ninaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba Yesu Kristo Ambaye alitoa hiyo

ahadi.

Kama nilivyosema katika ujumbe wangu wa mwisho, nikiwa nimesimama kule juu ya ukuta huo, nilipokuwa hapa majuma machache yaliyopita. Kila wakati unaposogeza kidole chako, hicho kinazunguka na kuzunguka ulimwengu, kamwe hakitakoma. Kila hatua unayofanya, utaiona kwenye Hukumu. Televisheni inathibitisha ya kwamba kiko hapa, kiwango cha nne. Maana, televisheni haiitengenezi picha hiyo, inalielekeza tu hilo wimbi kwenye tyubu, nawe unaona picha. Rangi, kila kitu, kila kitu kinachotembea kinachotendeka ulimwenguni, kinazunguka moja kwa moja kupitia hapa sasa, kikifanya rekodi. Siku moja, rekodi yako itafungwa, nawe utajibu rekodi hiyo. Hiyo ni kweli.

Mungu, jalia niunganishwe kabisa, jalia nife kabisa kwa nafsi yangu na chochote kinachonizunguka, bali nilitambue Neno la Mungu linaloishi miongoni mwetu leo hii!

Hebu na tuombe.

55 Bwana Yesu, Wewe ni kitendawili, wakati Mungu alipofanyika mwili. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe alasiri ya leo, ukituthibitishia hapa leo. Si kututhibitishia tu ... Kuna, nadhani, asilimia tisini, ama zaidi, ya watu walioketi hapa, wanaamini hilo, kila Neno. Bali ili tukuone tena, na utujalie kujua ya kwamba Neno hili ulilonena, ambalo lingali linasafiri kuzunguka na kuzunguka ulimwenguni, kama tu kumbukumbu, jalia tuingie kwenye kumbukumbu hiyo, leo hii, Bwana. Jalia tuingie ndani wala tusilisikie kana kwamba tu lilikuwa likija kupitia kwa mwingine, kutoka kwenye kinywa cha mwanadamu; bali jalia kinywa hicho, na mtu na watu, wote wanaoketi hapa, wafanyike Neno Lako. Tuko tayari kufa, Bwana, kwa mawazo yetu wenyewe, kukuona tu ukitimiza ahadi Yako, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Ninaomba ya kwamba utatujalia hili katika Jina la Yesu. Amina.

56 Kabla tu hatujaitisha mstari wa maombi. Nilikuwa nikilima barafu kidogo siku moja, pamoja na rafiki yangu mzee daktari. Akasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani, Billy."

Nikasema, "Vema."

Kasema, "Je! Unaamini katika ..." Hapo ndipo nilipopata wazo hili, kitendawili. Kasema, "Je! Unaamini katika kitendawili?"

Nikasema, "Hakika."

Akasema, "Na—najua unaamini." Akasema, akaniambia kuhusu mtu fulani aliyekuwa ameponywa, alikuwa ameombewa; ambaye alikuwa amemwuzia dawa za kifafa, kwa miaka kadha, wakati mwingine wangeshikwa na kifafa mara saba ama mara nane kwa siku; dawa kali. Naye akasema, "Hawakurudi tena. Nami huwaona wakati wote; kamwe hawakushikwa nacho tena." Kasema, "Ninataka kukwambia jambo fulani, kukujulisha tu ni—ninaamini yale unayonena."

57 Akasema, "Katika wakati wa kuzorota kwa uchumi, mwanangu hapa sasa alikuwa huko dukani." Kasema, "Yeye alikuwa—alikuwa akimngojea kijana fulani, alisema tu yeye ... Walikuwa wamesimama kwenye mstari, kwa ajili ya dawa." Kisha akasema, "Mtu mmoja alikuja hapa, naye alikuwa na mkewe," kasema, "mwanamke mdogo, yeye alikuwa ... Ungeweza kumtazama na kuona alikuwa karibu kujifungua wakati wo wote, mtoto." Kisha akasema, "Yeye hangeweza tu kusimama kwenye mstari huo tena, kwa hiyo a—akamleta mkewe mlangoni, na akiegemea tu bega lake."

Kisha akasema, "Mvulana wangu alipanda, kasema, 'Naweza kukusaidia?' Kasema, 'Naam,' kasema, 'haya hapa maagizo kutoka kwa daktari. Lakini, 'kasema, 'Ninataka kuwajulisha wazi.' Kasema, 'Mimi ... hatuna fedha bado.' Kasema, 'Tutazipata kutoka wilayani, bali mke wangu kamwe hawezi kuvumilia zaidi. Daktari alisema angepata dawa hiyo mara moja.' Kisha akasema, 'Kama utampa tu dawa, nitaenda moja kwa moja pale na kusimama kwenye mstari mpaka ni—nitakapopata fedha kutoka wilayani.'

"Na yule mvulana akasema, 'Bwana, samahani.' Kasema, 'Ni kinyume cha sheria zetu—zetu hapa, kutoa dawa bila kuwa na fedha.' Mnajua jinsi hali ilivyokuwa katika siku hizo. Kisha akasema, 'Ni—ninamhurumia, lakini siwezi kufanya hivyo.'"

58 Kasema, "Nilikuwa nimeketi nyuma hapa nikisoma gazeti. Ndipo nikaangalia juu, na," kasema, "kitu cha ajabu kiliuchochea moyo wangu." Kasema, "Nilitembea, nikasema, 'Ngoja kidogo, mwanangu, ngoja kidogo.' Mtu huyo akaanza kutoka mlangoni, akasema, 'Vema, sawa, mwanangu,' akaanza kutoka mlangoni." Kisha akasema, "Nilisema, 'Hebu kidogo,' kasema, 'hiyo ilikuwa ni nini?' Akasema, 'Vema, mtu huyu ...' Akamwelezea."

Akasema, "'Hebu nione maagizo hayo.' Kasema, 'Ngoja kidogo, mwanangu, nitakupatia dawa.'"

Kasema, "Nikarudi na kuchanganya maagizo hayo daktari alikuwa ameagiza kwenye karatasi yake." Kisha akasema, "Nilienda kule, na nilikuwa na hizo pesa." Kasema, "Nikamkabidhi, pasipo kujua kama nitazipata ama la, bali niliwazia tu nitazipata." Kasema, "Nilijisikia tu ya kwamba inanipasa kufanya hivyo." Kisha akasema, "Billy, nilipoiweka hiyo—hiyo dawa mkononi mwa mwanamke huyo," kasema, "ilikuwa ni

Bwana Yesu." Kasema, "Nilimwona Mtu fulani amesimama pale." Naye akasema, "Nilisoma baadaye, ya kwamba Maandiko yalisema, 'Kadiri mlivyowatendea walio wadogo wa hawa, watoto Wangu, mmenitendea Mimi.'" Akasema, "Billy, ni kitu gani kilitendeka kwa macho yangu? Je! Kweli niliuona?"

Nikasema, "Naam, bwana. Ninaamini jambo hilo. Ninaamini kwamba kweli ulitimiza wajibu wako kama mwuza dawa, katika mahitaji hayo ya dharura. Yesu alisema, 'Yale mliowatendea hawa wengine, mmenitendea Mimi.' Ninaamini hilo."

59 Nami ninaamini jambo lile lile leo, papa hapa liko pamoja na watu hawa, kwamba Yesu Kristo anaweza kujidhihirisha Mwenyewe, kujifanya Mwenyewe Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu alasiri ya leo. Mtaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Bwana awabariki.

Sasa tutaziita kadi za maombi, watu wapate kuja. Nasi hatuwezi kuwaleta wengi kupita kiasi, kwa kuwa nawazia sasa, kama ninaangalia saa vizuri, nina dakika ishirini na tano kufikia ambapo itatubidi kufunga kwenye saa kumi kamili, kwenye wakati mzuri, bali tutaendelea. Sasa hebu tuanzie kwenye kadi ya maombi, ninaamini ilikuwa A. Ilikuwa hivyo? A, hebu tuondoke kutoka A, moja.

Ni nani aliye na kadi ya maombi A, moja? Niwaite tu mmoja kwa wakati mmoja, kwa hiyo kama wewe ni kiwete tunaweza kukubeba. Vema. Kadi ya maombi A, moja. Ni nani aliye nayo, inua mkono wako, mahali fulani jengoni? Kadi, huko nyuma kabisa. Waweza kuja, mama, kama unaweza. Moja, mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? A, mbili, waweza kuinua mkono wako kama wewe ... Unaweza kutembea? Vema, njoni papa hapa, njoni upande huu. Tatu. Kama utauinua mkono wako mara moja, ni—ninaweza kukupata, haitatubidi kungojea kwa muda mrefu sana. Kadi ya maombi namba tatu, waweza kuinua mkono wako. Vema, mtu fulani kule chini. Vema, njoo huku, bwana.

Kadi ya maombi namba nne, waweza kuinua mkono wako upesi sasa, upesi tu uwezavyo. Kadi ya maombi namba nne. Vema. Namba tano. Mara tu ninapopiga simu, simama, namba tano. Vema. Namba sita, namba saba, namba nane, namba tisa, kumi—kumi. Sasa, moja, mbili, tatu, nne ... Kumi, sawa. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Ulikuwa unakuja, bwana, kumi na nne? Vema. Kumi na nne, kumi na tano. Vema, hilo, hilo litakuwa ... Hilo litatosha sasa hivi, hilo litatosha alasiri ya leo, maana hatuna wakati mwingi sana.

60 Sasa angalia. Ninawatakeni mnisikilize kwa makini. Sasa, Yesu alitoa ahadi hii, ya kwamba, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona." Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] "Ulimwengu," *ulimwengu*, ni "utaratibu wa ulimwengu." Mnaona, ya kwamba, Yeye alijua wangeondoka wakaingia katika mitindo na kadhalika. "Lakini hawatania tena, bali ninyi mtaniona." Kwa kuwa Yeye aliahidi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli? ["Amina."] Na Biblia ilisema, Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Unaamini jambo hilo? ["Amina."] Hiyo ni ahadi.

Sasa, si lazima uwe hapa juu, upate kuponywa. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuamini Neno hilo kuwa ni Kweli. Sasa nitawaomba, mkiweza, kuwa tu na kicho na utulivu kwa muda mfupi.

61 Je! Wote waliingia, Billy? Una wawili nje, watatu nje? Unasemaje? [Ndugu fulani anasema, "Watatu zaidi." - Mh.] Watatu zaidi? Namba tatu, kadi ya maombi namba tatu. Ni nini, vipi, ni neno gani la Kimeksiko kwa ajili ya hayo, matatu? Kuna mtu yeyote anayeweza kusema jambo hilo? [Mtu fulani anasema, "tres."] Vema, hakika walisikia. Ni nini, huyo, ye yote aliye na hiyo kadi ya maombi, aingie mstarini, sivyo? Loo, naam. Loo, nafikiri ilikuwa ni mtu fulani aliyekuwa nayo, wala hakujua, nao wakarudi nyuma. Vema. Sasa, sasa vipi kuhusu ...

Je, kila mtu anaamini sasa kwa—kwa moyo wako wote? Vema, hebu na tuombe tena basi.

62 Bwana Yesu, sasa tunatambua ya kwamba tunaweza kusoma Neno, kwa ujuzi wetu wote, kulielezea. Lakini, Bwana, Wewe ndiwe pekee unayeweza kulithibitisha. Wewe ndiwe pekee unayeweza kusema ya kwamba ni kweli ama si kweli. Na, Baba, ninaomba leo ya kwamba utayaacha macho ya watu yafunguliwe. Jalia tuone kitendawili alasiri ya leo, ninii tu, Bwana, cha kutosha kuwafanya watu waone kwamba Wewe upo, kwamba wewe hu—hujatoweka, kwamba Neno Lako ni lile lile jana, leo, na hata milele. Kwa kuwa, Wewe ndiwe hilo Neno. Kwa ajili ya wagonjwa, Bwana, kwa ajili ya wale wanaoteseka; wengi labda wako hapa kutoka sehemu mbalimbali nchini, sehemu za taifa, hawana budi ... wanateseka sana, wasingeweza kufurahia mikutano, vinginevyo, kama hawakuponywa. Ninaomba ya kwamba utawaponya. Jalia hilo, Bwana. Na sasa sisi ni wanadamu tu kimwili, na tunaweza tu kulihubiri Neno na kusema yale uliyosema kwamba ni Kweli, sasa Wewe Ndiye wa kulifanya halisi. Ninaomba ya kwamba utatujalia, katika Jina la Yesu. Amina.

63 Sasa ningetaka tu kwa usikivu wenu usiogawanyika, kwa muda kidogo tu, na kama kila mtu ataketi tu sasa kwa dakika chache. Sasa, kadiri ni juavyo mimi, bila shaka, simjui mtu yeyote ambaye ninaweza kumwona humu—jengoni, ambaye ningemjua huko nje. Sasa, si lazima uwe hapa upate kuponywa, mtu yeyote anajua jambo hilo. Mnaona?

Kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, asingeweza kupata kadi ya maombi, tungesema, naye aligusa vazi Lake. Ndipo akageuka na kuangalia, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Nao wote wakakana jambo hilo. Naye akaangalia kila mahali na kumwona maskini mwanamke huyu. Hakuweza kujificha, maana, mnaona, Roho wa Mungu, aliyekuwa ndani Yake, alimwongoza. Yeye alikuwa Neno. Nalo likamwongoza mpaka kwake, ndipo akamwambia shida yake ilikuwa nini. Alikuwa akitokwa na damu, naye akaponywa. Aliamini. Na mara, mwilini mwake, akajisikia ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumezuiliwa, (hiyo ni kweli?) kulikuwa kumekoma papo hapo.

64 Sasa Yeye ni yeye yule leo. Si lazima uwe hapa. Sasa, Biblia ilisema ya kwamba katika Agano Jipya sasa, ya kwamba, "Yesu Kristo ndiye Kuhani wetu Mkuu." Je! Tunaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Kuhani Mkuu pekee tuliye naye, Mwombezi pekee tuliye naye kati ya Mungu na mwanadamu, ni yule Mtu, Kristo Yesu. Unaamini jambo hilo? ["Amina."] Na Biblia ilisema, "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." Hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Inua mkono wako kusudi ... Vema. Mimi siko miongoni mwa wageni, kwenye Neno hili.

Sasa angefanyaje kama ulimgusa? Yeye angefanya vile vile alivyofanya wakati alipokuwa hapa, kwa sababu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

Sasa amini tu. Sema tu, "Sasa, Bwana, nimekuwa kwenye mikutano niliyohudhuria, lakini nitaamini tu, leo. Mimi—hata sitajifikiria mwenyewe. Nitaamini tu kwa moyo wangu wote, ya kwamba Wewe upo hapa. Nami nina haja, na Wewe tu ... Wewe nisaidie, Bwana." Mnaona? Sasa fanya hivyo. Msiwe na wasiwasi; tu—tulieni tu kwa uaminifu.

65 Karama ya imani si kitu unachochukua na kufanya kitu fulani nacho. Karama ya imani ni kujiondoa tu njiani. Karama ni kujiondoa njiani.

Sasa hapa amesimama mwanamke. Baba Mungu anajua, kadiri nilivyopata kujua, sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Lakini, wala hakuna yapata watu wawili ama watatu ninaoweza kuwaona huko, niwajua.

Nafikiri huyu ni Bibi Vayle anayeketi hapa, mke wa Ndugu Lee. Sina hakika. Ndipo ninajua hawa wavulana watatu ama wanne wanaoketi papa hapa. Kadiri nijuavyo mimi, hayo tu ndiyo ninayoona mkutanoni wakati huu, ninajua. Ninaamini huyo ni Ndugu Anthony Milano anayeketi pale, kutoka New York. Ndugu Pat Tyler kutoka Kentucky. Nje ya hayo ... Ninajua Fred Sothmann yuko mle mahali fulani, nilimsikia akipaza sauti "amina" muda mchache uliopita. Hilo, hilo ni karibu kikomo, na Baba wa Mbinguni anajua hilo.

66 Na mwanamke huyu amesimama hapa, wala sijapata kumwona. Sijui yeye yuko hapa kwa sababu gani. Yeye ni mwanamke tu aliyekuja hapa jukwaani, kama vile wewe ulivyoketi huko nje.

Sasa, kama mwanamke huyu ana haja, vema, basi mimi—mimi, kama ningeweza kumsaidia, hakika ni —ningemsaidia. Lakini sasa mimi—mimi ... Hiyo inategemea anahitaji nini. Kama ilikuwa ni pesa, huenda ni —nikajitahidi sana kumtafutia dola tano ama kumi. Nje ya hayo, sijui, mnaona, nisije nikampa hundi iliyoahidiwa, mpaka nitakapopata mshahara wangu mwezi ujao. Lakini sasa vipi kama ana shida ya nyumbani? Ndipo ningesema, "Nenda kamwite mumeo, hebu tuzungumze pamoja, labda naweza kukusaidia. 'Sina njia ya kufika nyumbani'? Vema, nitamwomba mtu fulani kama watakupeleka, wakupeleke nyumbani, wanaopitia njia yako. Unaishi kwenye mtaa gani hapa chini?" Ama cho chote kile, sijui. Lakini kama ni ugonjwa, basi si—sijui. Mnaona? Lakini simjui mwanamke huyo.

Lakini kuna Mtu fulani hapa, Neno hili, aliyeahidi, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya."

67 Sasa, labda, vipi kama mwanamke huyu ni mgonjwa, labda ana kansa, labda ana TB, na, ama kitu fulani ambacho dawa haiwezi kusaidia katika—katika hatua hii? Vema, sasa, nisingeweza, kwa vyo vyote vile nisingeweza kumponya mwanamke huyo.

Lakini sasa kama Yeye anaweza kunifunulia kile anachotaka, kama tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, ama kama alivyomwambia Nathanaeli, ama—ama kumwambia Simoni jina lake ni nani. Kasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona. Tangu sasa utaitwa Petro, ambalo linamaanisha 'jiwe dogo.'"

Vema, sasa, kama Yeye angefanya jambo kama hilo hapa mbele ya ninyi nyote, hilo linaonyesha ya kwamba Neno hilo ni Kweli. Sasa, ni wangapi watakoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Kuna mtu yeyote hapa anayemjua mwanamke huyu, inua mkono wako, watu wo wote humu jengoni? Naam, wengi wenu mnamjua. Vema. Naye Baba anajua ya kwamba sijui. Vema, sasa, hebu tuone tu Yeye angesema nini. Na hilo, hilo lingekuwa ni kitendawili? ["Amina."] Sijui ana shida gani. Sijui yeye yuko hapa kwa ajili gani, wala chochote kumhusu. Lakini Mungu anajua jambo hilo.

68 Nitazungumza na mwanamke huyu. Sasa huyu ndiye mtu wa kwanza niliyekuwa naye kabla yangu,

kwa yapata miezi mitatu. Sasa nataka tu kuzungumza na mama huyo, kwa muda kidogo tu. Na hiyo ni nini? Wasiliana na roho yake. Kama tu vile Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, wasiliana na roho yake.

Sasa, kama Bwana Yesu, mama, anaweza kunifunulia shida yako, ama kilichokuleta hapa, ama jambo fulani kukihusu, ambalo unajua ya kwamba sijui lolote kulihusu, ama kitu kama hicho, je! ungeamini ilikuwa ni Yeye? Ingekuwa ni Yeye, sivyo? [Huyo dada anasema, "Naam." - Mh.] Ingekuwa ni Yeye. Kama atafanya jambo hilo, basi sote tutashukuru kwamba tunajua tunaninii ... ya kwamba Neno Lake ni kweli, basi tunaweza kuweka matumaini katika jambo hilo.

Sasa, kama anaweza kufunua shida yako ni gani, kunifunulia mimi, nami sikujui, nawe unajua hilo; bali sasa kama Yeye anaweza kunifunulia shida yako ni nini, ama jambo fulani kukuhusu wewe, basi hiyo inaonyesha kwamba kuna Roho fulani hapa, mahali fulani, anayekujua, nawe unajua kwamba sikujui. Kwa hiyo isingekuwa mtu huyo, ingekuwa ni Roho. Na hivyo ndivyo Mungu alivyoahidi wakati huu wa Efeso. Je! Mnaamini jambo hilo kuwa ni Kweli? [Huyo dada anasema, "Naam, ninaamini." - Mh.] Na alijalie.

69 Ninaona jambo moja, anaugua kitu kama uvimbe hapa juu kichwani mwake. Hiyo ni kweli. Sivyo? Inua mkono wako kama ndivyo ilivyo. Lakini uvimbe usingekufanya upige chafya na uendelee namna hiyo, kwa hiyo una homa iletwayo na vumbi, pia. Hiyo ni kweli. Wewe hutoki Phoenix. Unatoka mahali ambapo kuna —kuna vilima vingi, miti. Umetoka Flagstaff. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? [Huyo dada anasema, "Naam." - Mh.] Wewe ni Bibi Earl. Naam. ["Sawa."] Ni kweli, sivyo? Sasa nenda, ukiamini, yote yatakwishia.

Sasa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Sasa, Baba wa Mbinguni anajua ndio kwanza tu nimwone mwanamke huyo. Mnaona Neno limethibitishwa. Sasa, si mimi, mimi ni mwanadamu tu. Ni kama tu maikrofoni hii, ni bubu bila mimi kuzungumza kupitia kwake, ama mtu fulani. Na vivyo hivyo mtu ni bubu tu. Lakini ni Roho, na Roho huyo yuko papo hapo miongoni mwenu. Mnaona? Yeye ndiye mponyaji, si mimi.

70 U hali gani, bwana? Mtu mwingine ambaye ni mgeni kwangu. Simjui mtu huyo. Sasa, ni juavyo mimi, sijapata kumwona maishani mwangu.

Lakini sasa Roho, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu na Yesu Kristo ni Roho yule yule. Aliyepakwa mafuta, Yesu, yule Mtu, alikuwa ni Mwana wa Mungu, bali Roho Mtakatifu aliyekuwa juu Yake alikuwa ni Mungu. "Baba Yangu anaka ndani Yangu." Mnaona, ni Roho Mtakatifu, kwa hiyo bado ni Mungu.

Sasa kama ningeweza tu kuninii, kama mtu huyo angeweza, kujiondoa njiani, basi sehemu hiyo imekufa, basi acha Roho wa Uzima aanze kutenda kazi. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu ninangojea kwa dakika moja, kuona kile kitakachotendeka mpaka upako utakapoanza.

71 Kama Bwana Mungu, ambaye tuko katika Uwepo Wake, atanifunulia, bwana, shida yako ni nini, ama kitu fulani ambacho umefanya, ama—ama jambo fulani kukuhusu wewe, jambo fulani tu. Bila shaka, tungezungumza zaidi, ndivyo ingekuwa zaidi. Lakini, mnaona, kuna wengine wamesimama kwenye mstari. Lakini kama Yeye ataniambia tu shida yako ni nini, utaamini mimi kuwa mtumishi Wake, na kuamini Yeye yupo? [Ndugu huyo anasema, "Ndiyo.] Henia. Hiyo ni kweli? ["Hakika ni kweli. Naam."] Sawa.

Sasa unasema, "Hilo lilifanyikaje?" Laiti ningalijua. Hakuna mtu anayeweza kulielezea hilo. Hicho ni kitendawili. Mnaona?

Hapa, kusudi upate kujua, nimeona kitu kingine, kuchunguzwa; una ugonjwa wa moyo, pia. Inua mkono wako. Bw. Anderson, unaweza kwenda nyumbani sasa, Yesu Kristo atakuponya. Hiyo ni kweli. Amini tu, uwe na imani. Usitilie shaka.

72 U hali gani, bwana? Hatufahamiani. Sikujui. Nijuavyo mimi, ni mara ya kwanza niliyopata kukuona, kukujua. Hiyo ni kweli. Lakini Yeye anatumia, sote wawili.

Sasa mnajua ni kwa nini haya yanatukia? Ni neema Yake ikiruhusu jambo hilo, kwamba ingewafanya watu hawa wamjue Mungu. Sasa, bila kujua lo lote kukuhusu wewe, hata sikujui hata kidogo, ni mgeni tu aliyekuja hapa. Sasa ingekuwa ni kitendawili kabisa kwa jambo fulani kutukia, ku—kujua ulikuwa na shida gani, ama jambo fulani ulilokuwa umefanya, ama jambo fulani usilipaswa kufanya, ama jambo fulani ulilipaswa kufanya, ama wewe u nani ama jambo fulani kukuhusu. Ingebidi iwe ni kitendawili, maana hakuna njia kwa mtu ye yote kujua jambo hilo, nje ya ufunuo fulani wa yasiyoonekana. Hiyo ni kweli. Sasa kama Yeye atakufanyia hilo, kati yako na mimi, ili kwamba wasikilizaji...sio maonyesho, bali kwamba wapate kuona Wa—Waefeso iko hapa, kwamba hiki ndicho kitu kinachounganisha dhehebu na Nchi yenye Utukufu. Yeye aliahidi jambo hilo, ili wapate kuhakikishiwa ya kwamba yale tunayosema ni Kweli.

Sasa kukujua wewe, unajua sikujui. Hiyo ni, inua mkono wako ili watu waone ya kwamba wewe ... Mimi, sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu. Yeye ni mwanamume tu anayesimama hapa. Uliza ye yote wa hao wengine. Lakini anaugua heria. Pia una bawasiri. Hiyo ni kweli. Umetoka mbali sana,

kufika hapa. Wewe hata si Mmarekani. Wewe ni Mkanada. Ulileta mwana aliye na ugonjwa wa akili. Hiyo ni kweli. Mnataka nikwaambie unakotoka? Umetoka mkoa wa Saskatchewan, mji wa Saskatoon. Amini kwa moyo wako wote, na Mungu atakurudisha nyumbani ukiwa mzima, pamoja na mwanao, kama unaamini. Unaamini jambo hilo? Mungu akubariki.

Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Bwana Mungu angali ni Mungu. Mnaona? Hakuna mwingine ila Yeye.

73 U hali gani? Huyu hapa bibi, mgeni kwangu, labda mkubwa zaidi kidogo. Sijawahi kumwona; bali yeye ni—yeye ni mwanamke tu anayesimama hapa. Itanibidi kuharakisha, maana nina dakika saba ama nane tu sasa, mnaona. Angalia tu hapa. Je! Unaamini ya kwamba mambo haya ni kweli? Kwa moyo wako wote? Unajua haiwezekani kwangu kujua shida yako, ama cho chote kukuhusu. Bali si jambo lisilowezezana kwa Mungu kujua, kwa kuwa Yeye alijua hata kabla ulimwengu usijakuwapo. Hiyo si ni kweli? [Huyo dada anasema, "Hiyo ni kweli." - Mh.]

Ni wangapi wanaamini hilo kuwa ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Hakika. Yeye alijua kila wakati ambapo ungepepesa jicho lako. Yeye hana kikomo. Na hebu wazia tu; kwa neema Yake Yeye amewasilisha, pamoja na Injili Yake, jambo lile lile aliloahidi kufanya. Halafu kuna Mbingu, nasi tutaifikia. Nasi tuko katika Efeso hii sasa hivi. Tuko katika hili, kutoka kwenye moja, kuingia jingine.

Una matatizo mengi sana, matatizo, matatizo mengi sana. Nawe hutoki hapa. Umetoka magharibi ya hapa. Umetoka California. Hiyo ni kweli. Wewe pia una mwana anayeteseka. Hiyo ni kweli. Ninyi ... Kuna kitu fulani, ninaendelea kuona maji ama ziwa kubwa mno. Loo, ni, una—una mtu aliye karibu nawe, anayeishi Chicago, ambaye ananijua. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sasa, unajua sikujui, lakini unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bi McGuire. Una ombi lako. Nenda nyumbani ukimshukuru Mungu.

U hali gani? Wewe ni kijana mwenye nguvu.

74 Lakini magonjwa na maradhi hayana upendeleo. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Tunajua tu ya kwamba si kumheshimu mtu.

"Kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote!" Pumu hiyo ingekuacha kama ungeamini kwa moyo wako wote.

Shida ya kifua, unaamini ingekuacha, pia, dada, nawe ungepata afya? Uligusa nini? Yeye yuko futi ishirini kutoka kwangu, ama zaidi. Alimgusa Bwana. Ni msongamano, wa neva. Utakuwa mzima.

Hili ni jambo zuri sana ambalo msichana huyu anasimama hapa kwa ajili yake. Yeye ni mgeni moja kwa moja. Sijawahi kumwona mwanamke huyu. Lakini yeye ameletwa hapa na mtu mwingine. Na kinachomleta hapa, ni kwa sababu alisikia kanda niliyotengeneza. Naye yuko hapa akitaka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo hasa lililomleta hapa. Hiyo ni kweli, msichana. Hiyo ni kweli. Njoo hapa.

Mungu mpenzi, jalia mtoto huyu anayesimama hapa, anayetoka gizani aingie Nuruni, jalia ampokee Roho Mtakatifu; nenda nyumbani kwake na wapendwa wake, uwaonyeshe mambo makuu ambayo Yesu amemtendea. Amina.

Mungu akubariki. Usitilie shaka. Amini.

75 Mungu anaweza kuponya kila namna ya wasiwasi na (unaamini hilo?) hali ya pumu, na kukupa afya. Unaamini jambo hilo? Basi nenda zako, amini kwa moyo wako wote. Mungu na akubariki, ndugu.

Una umri gani? [Huyo dada anasema, "Thelathini na nane." - Mh.] Huna budi kutoka kwenye wasiwasi huo kabla ya muda mrefu sana, sivyo? Una hali za kuishiwa nguvu za kila namna, na una matatizo ya kila namna. Bali yamekuacha sasa. Naam, bwana.

Mungu huonya wasiwasi, ugonjwa wa tumbo, pia. Unaamini jambo hilo? Basi nenda ukale unachotaka. Yesu Kristo alikuponya.

Mnaamini huko nje, kila mmoja wenu? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

Kuna mtu ameketi akiwa na—na shati, akiniangalia, naam, aliangalia shati lake chini wakati huo. Naam. Je! Unaamini Mungu anaweza kuponya shida ya tezi, anaweza kukuponya? Ulikuwa ukiamini wakati huo (sivyo?), Wakati uo huyo mvulana huyu mdogo alipoponywa hali hiyo ya pumu. Nenda nyumbani, mpenzi, utakuwa mzima, pia, unaona. Amini kwa moyo wako wote.

Binti mdogo anayeketi karibu na mke wako pale, je! Ungeweza kuamini macho yako yatapona, pia? Unaamini ya kwamba Mungu ataponya ugonjwa huo wa jicho? Inua mkono wako kama hilo ndilo ulilokuwa ukiombea. Mnaona?

Waligusa kitu gani? Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

76 Unaamini? Unaamini, ewe kijana? Mungu anaweza kuponya hiyo hali ya damu, kuifanya sawa, (utaamini jambo hilo?) Kuondoa hicho kitu cha kisukari na kukupa afya. Unaamini jambo hilo? Nenda ukamwambie unaamini, na uende.

Njoo, bwana. Una shida ya tumbo. Je! Unaamini Mungu anaweza kuuponya, upate afya? [Ndugu huyo anasema, "Naam, ninaamini." - Mh.] Nenda zako, liamini; utakuwa mzima, utakuwa mzima.

Njoo, mlete huyu mvulana mdogo. Angalia hapa, mwanangu. Umetoka mbali sana. Wakati mwingine badiliko katika mwinuko, badiliko katika hali ya hewa, litafanya hivyo, kuponya hali ya pumu. Lakini kuna uponyaji mmoja wa hakika, Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Yeye alimtoa Mwanawe, ili kwamba wako apate kuponywa. Unaamini jambo hilo? Liamini kwa moyo wako wote, nalo litamwacha. Atakuwa mtu wa kawaida, mzima. Mungu akubariki, dada.

Unaamini? Je! Mungu bado anafanya vitendawili? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Mambo yasiyoelezeka, yasiyoeleweka, mambo ambayo watu wasingeelewa jinsi yangekuwa, lakini bado ni kweli, sivyo? ["Amina."] Sasa ni wangapi wanaohisi, na kujua rohoni mwako, ya kwamba hapana budi kuweco na kitu Fulani hapa ambacho kimepita ufahamu wa mwanadamu?

77 Sasa, nafikiri tuliita angalau watu kumi na watano kwenye mstari huo, kila mmoja wao; na wanne ama watano, sita, pale mstarini, wasio na kadi za maombi, ama vyovyote walivyokuwa pale mstarini, huko kwenye wasikilizaji pale. Lakini tuko sasa hivi dakika moja tu ya wakati, wa kufunga.

Je! Yeye alifanya hivyo jinsi hasa alivyosema angefanya? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Sasa ni wangapi wanaoamini Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, wakihisi Uwepo Wake? ["Amina."] Sasa mmeona Uwepo Wake. Sasa jicho lako limeona, masikio yako yamefahamu, na Mungu amethibitisha, mbele ya macho yako, Uwepo Wake. Na huo ndio unaouhisi wakati wote, unaokuhukumu wakati umekosea, na kukwambia usifanye hivyo, Mungu yuyo huyo ameweza kuonekana kwenu hapa alasiri ya leo, katika matendo Yake. Ni wangapi wanaosema "amina" kwa jambo hilo? ["Amina."] Hakika, ndivyo ilivyo. Sasa Yeye yuko hapa.

78 Kuna mmoja hapa kati yetu, ambaye hajawahi kuwa Mkristo; hajawahi kuungama kamwe, kamwe hajaenda kanisani? Ungeweza kusimama, na kusema, "Ninataka kusimama, si kwako, mhudumu; bali ninataka kusimama nikiwa katika Uwepo wa Mtu huyu, Yesu Kristo, ambaye ni Roho Mtakatifu juu yetu sasa. Ninataka kusimama na kusema, 'Ninataka Wewe uniokoe na dhambi zangu'?" Hilo tu ndilo ninalotaka ufanye, simama tu, na hilo litashuhudia. Hivyo tu ndivyo tulivyo na wakati wa kufanya. Sema, "Nataka kuwa Mkristo." Simama kwa miguu yako, kisha uketi moja kwa moja chini.

Kuna mmoja humu jengoni? Ni wangapi walio jengoni? Sipaswi kusema, "Kuna mmoja?" Maana huenda kukawa na zaidi ya mmoja. Ni wangapi jengoni watasimama sasa hivi, na kusema, "Nimekuwa makosani, Mungu. Nisamehe. Nitainuka nikupe ushuhuda ya kwamba nimekosea. Nitaketi chini nikiwa hapa katika Uwepo Wako. Nitaketi chini?" Simameni tu.

Kuna mmoja, kuna zaidi ya mmoja? Mkono mmoja. Mungu akubariki, kijana. Kuna mwingine? Mungu akubariki. Kuna mwingine? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Kunaye? Mungu akubariki, huko nyuma. Kuna mwingine, "Nimekuwa makosani. Mungu, nisamehe?" Mungu akubariki, bwana. "Nimekuwa makosani. Na—samahani, Bwana." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

79 Kuna mtu ye yote ambaye amekuwa akishuku huduma hii, nawe umeshawishika sasa ya kwamba ni kweli? Inuka pale, na useme, "Mungu, nisamehe." Inua tu mkono wako, useme, "Ni—nilikuwa na mashaka kidogo, Ndugu Branham; yote yamekwisha sasa." Inua mkono wako. Si hata mmoja? Asanteni.

Ni wangapi wanaoamini Hili? Isingekuwa mimi; bali ni Kristo, Mwana wa Mungu. Asanteni. Ndipo utaona mambo makuu kuliko haya yakitendeka, mradi tu utaamini. Dumu tu na Kristo. Nitajitahidi kadiri niwezavyo kudumu pamoja Naye, mimi mwenyewe.

Sasa ni wangapi hapa walio wagonjwa na wahitaji, inua mkono wako, "Mimi—mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham, mimi ni mhitaji?" Mnaona, waangalie tu watu. Sasa mtafanya jambo hili na kuamini tu neno langu kiasi hiki? Hebu na tuwekeane mikono sisi kwa sisi, huku nikiinyosha mikono yangu kuwaelekea.

Hebu na tuombe.

80 Mungu mpenzi, ninakuletea wasikilizaji hawa wachache, alasiri ya leo, ambapo tumesikia na kusoma Neno la Mungu. Tunajua ya kwamba kila kitu ni Kweli, kwa sababu ni Neno Lako. Hatujaamini tu sasa kwamba ni kweli; tunajua ya kwamba ni kweli. Tumekuona Wewe, Bwana, ukifanya jambo fulani ambalo litawafanya watu wajue ya kwamba bado kuna ... Mbali na kitendawili cha—cha ulimwengu, na anga, na kanuni za kawaida za Mungu, tunaweza kuona hapa ambapo kanuni za mauti zinafanya kazi katika mwili wa mwanadamu, ambapo sayansi imeshindwa ku—kuponya kwa utafiti wao. Na, Bwana, tunashukuru kwa ajili ya watu hao. Sisi kamwe hatuwadharau. Tunashukuru kwa ajili yao. Lakini, Bwana, inapofikia mahali ambapo hawawezi kufanya la zaidi, sasa tunauona mkono Wako mkuu ukiingia; tukijua ya kwamba

hakuna mtu angeweza kuwaponya, kwa kuwa angekuwa ni daktari, ama imbidi kuchukua tiba fulani. Lakini kumwona Mwana wa Mungu akishuka, na hiyo ilifanya ahadi, kwamba sisi sote tunaamini.

81 Na kila mtu aliinua mkono wake, ambao hawakuokolewa, na—na walitaka kuokolewa. Mungu, kitu fulani kiliuonya moyo wao. Baadhi yao walisema "walikuwa wamekosea," labda walirudi nyuma na walitaka kurudi. Ninaomba ya kwamba utamrudisha kila mmoja. Kwa kuwa wanajua, Bwana, na kujua ... Wengi wao huenda walinijua mimi, ama kunifahamu mimi, kwa miaka hii, na wanajua ya kwamba hakuna kitu kizuri ndani ya mtu, na hasa mimi. Ingewezekanaje kuwe na jambo lolote zuri? Lakini hata hivyo waliona Neno hilo, ambalo Mungu aliahidi, likidhihirishwa. Wao wameshawishika ya kwamba ni Kweli. Wamekubali jambo Hilo.

Wengi hapa nisingeweza kuwaleta jukwaani. Na, Baba, Wewe unanishuhudia, kamwe sijapata kusema ya kwamba lingekuwa ni jambo ambalo ningeweza kufanya, si zaidi ya kujitolea mwenyewe Kwako, na kukuacha Wewe uniondoe njiani na kuiweka Roho Yako mle ndani ikatende kazi. Sasa, Baba, tukiona kuwa mtu mmoja anaweza kufanya jambo hilo, mwingine anaweza kufanya, ninaomba ya kwamba kila mtu aliyeweka mkono wake juu ya mwingine, aliye mgonjwa na anayeteseka, ataponywa wakati uu huu.

Jalia Roho Mtakatifu mkuu apitie jengoni sasa hivi na kumpa kila mtu afya. Mwokoe kila mtu, Bwana. Toa tukio kama hilo. Mimina Roho Mtakatifu, Bwana, juu ya wasikilizaji hawa. Loo, tunakutazamia kufanya mambo makuu juma hili lijalo. Hebu na iwe hivyo, Bwana, sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo.

82 Sasa hebu sote na tusimame kwa miguu yetu. Je! Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa nashangaa kama dada yetu, kwenye piano pale, angetupa sa—sa—sauti ndogo ya hii, "Nitamsifu. Nitamsifu." Mmesikia hayo? Sasa hebu na tuimbe, pamoja. Sasa tutatarajia kukutana nawe kesho jioni. Sasa tutaondoka rasmi, katika dakika moja, bali ninataka kuimba wimbo huu pamoja nanyi. Vema, hebu twende.

Nitamsifu, (hebu tuinue mikono yetu) Nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi ya kutawanyika. Vema, Ndugu Jewel Rose atatutawanya. Mungu akubariki, Ndugu Rose, wakati tukiwa na ninii yetu ...



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7